

Pambazuko

Toleo Namba 181

Jumatatu, Septemba 7-13, 2026

Pambazuko laripoti, Samia akerwa uchafu Dar Uk. 14

Lissu 'ahutubia' taifa kutoka kizimbani

Uk. 6&7

- Atumia Mahakama kuwa jukwaa la ujumbe wa kisiasa



CCM: Tunaomba Mungu Polepole apatikane hai

Habari Uk. 13



Kigogo Udasa ahofu Katiba Mpya, aibua Tanganyika

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Wataaaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam (Udasa), Dkt. Dominicus Makukula, haamini endapo Katiba Mpya itapatikana kabla ya mwaka 2030.

Habari Uk. 12



Jicho la Tai

Uhamisho wa magavana siyo sabuni ya makosa yao



Safu Uk. 5

Kujiuzulu Dkt Nchimbi mwisho au mwanzo wa mgogoro?

Habari Uk. 20

Tafakuri ya Bagonza

Jaji mkuu na mahakama zetu

Safu Uk. 10

Wafanyakazi IPTL waiangukia serikali iwalipe

Habari Uk. 15

■ Tahariri

Usafi usisubiri filimbi ya Rais Samia

KAULI ya Rais Samia Suluhu Hassan kukemea uchafu uliokithiri katika miji yetu, hasa Dar es Salaam, inapaswa kuwatafakarisha kwa kina viongozi na watendaji wa serikali katika ngazi zote.

Septemba 2, 2026, Rais Samia aliwataka wakuu wa mikoa kusimamia usafi na kuondoa wakandarasi wasio na uwezo wa kufanya kazi za umma kwa ufanisi na ubora.

Hata hivyo, pamoja na karipio, lakini swali kubwa linabaki; kwa nini lazima Rais Samia aseme ndipo viongozi walioajiriwa kwa kazi hiyo waamke na kuanza kukimbizana, ina maana hawaoni uchafu kwenye maeneo yao?

Tuna wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa afya, watendaji wa kata, mitaa, vitongoji na vijiji. Wote wana mamlaka, ofisi, bajeti na mishahara, hata hivyo, ni kama hawafanyi kazi.

Inashangaza wanaona kabisa kwamba taka zinaziba mifereji, masoko yananuka, mitaro inageuka dampo na maeneo ya makazi yanazungukwa na uchafu, lakini hawa wakubwa wetu wanaendelea kukaa ofisini wakiburudishwa na viyoyozi kana kwamba tatizo hilo linamhusu Rais Samia pekee.

Hali hii ni aibu. Rais hawezi kuwa afisa usafi wa kila mtaa. Hawezi kutoka Ikulu kwenda kugagua pipa la taka, mfereji uliozibwa au jalala lililoachwa katikati ya soko, haya ni majukumu ya wengine.

Viongozi wa maeneo yao wanaposubiri “maagizo kutoka juu” ndipo wachukue hatua, basi umma unapaswa kujiuliza uwezo wao wa kuona, kupanga na kuwajibika unaanzia wapi na kuishia wapi?

Uchafu siyo dosari ya sura ya mji pekee. Ni tishio kwa afya, mazingira, biashara na heshima ya taifa. Mifereji iliyozibwa huongeza mafuriko. Taka zinazooza huvutia nzi na wadudu, huku maji machafu yakichochea magonjwa.

Pambazuko linatambua kwamba serikali hutumia fedha nyingi kutibu matatizo ambayo yangeweza kuzuiwa kwa usimamizi wa kawaida,

ratiba thabiti ya ukusanyaji taka na utekelezaji wa sheria bila upendeleo.

Sisi tunawataka viongozi hawa watoke kwenye viti vyao. Watembelee masoko, stendi, mitaa na maeneo ya kutupia taka. Wakague mikataba ya wakandarasi, wafuatilie magari ya taka na waeleze wananchi mapato ya ada za usafi yanavyotumika.

Mkandarasi asiye na vifaa aondolewe; mtendaji anayefumbia macho uchafu awajibishwe. Urafiki, undugu au maslahi ya kisiasa yasiwekwe mbele ya afya ya wananchi.

Ileweke kuwa uongozi wa eneo maana yake ni kugundua tatizo kabla halijafika Ikulu. Kila halmashauri iweke ramani ya maeneo hatarishi, ratiba zinazoonekana hadharani na namba za kupokea malalamiko.

Wakuu wa mikoa na wilaya wapimwe kwa matokeo, siyo hotuba. Vikao vya usafi visiishie kwenye makabrasha; vitoe majina ya waliowajibika, hatua zilizochukuliwa na muda wa kurekebisha kasoro. Bila hivyo, uzembe utaendelea kulindwa na ukimya wa ofisi zetu kila siku.

Wananchi nao wana wajibu wa kutotupa taka ovyo, kulipa ada halali na kutoa taarifa wanapoonza uzembe, lakini huwezi kumlau mu mwananchi pekee wakati taka hazikusanywi, mapipa hayapo na mifereji haisafishwi. Uwajibikaji lazima uanze kwa wenye mamlaka.

Rais Samia amepiga filimbi na sasa hatutarajii kuona usafi wa siku mbili kwa ajili ya kamera, kisha uchafu urudi baada ya “vumbi kupoa,” tunataka mifumo ya kudumu, malengo yanayopimika na taarifa za wazi kwa umma.

Kiongozi anayeshindwa kutatua hata tatizo linaloonekana, atatuaminisha vipi kwamba anaweza kusimamia maendeleo makubwa? Kama kazi yake ni kusubiri mshahara na agizo la Ikulu, basi hana sababu ya kuendelea kushikilia ofisi ya umma. Aondolewe.

Biashara ya Matunda... ■



Msimu wa zao la zabibu umeanza huko Dodoma kwa wakulima, matunda hayo sasa yanapati-kana kwa wingi katika maeneo mengi. Kamera ya Pambazuko jana ilinasa baadhi ya wa-chuuzi wa ma-tunda hayo eneo la Mwembechai, Dar es Salaam.

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

■ Dunia: Hapa na Pale

Alia na nguvu za kiume

MWANAUME mmoja Mkenya anataka matatizo kama vile ukosefu wa nguvu za kiume yatambuliwe kisheria kama ulemavu.

Katika ombi alilowasilisha bungeni, Dkt. Benson Kibore amesema tatizo la nguvu za kiume na ukosefu wa hamu ya kushiriki mapenzi, hali inayojulikana kama HSDD, linahitaji kushughulikiwa kupitia sheria na sera za afya.

Amesema matatizo hayo, ambayo hapo awali yalihusishwa zaidi na wazee, sasa yanaonekana pia miongoni mwa vijana.

Dkt. Kibore anarejelea utafiti wa 2026 uliofanywa Nairobi na kuchapishwa kwenye jarida la medRxiv, umeonyesha kuwa asilimia 10.4 ya vijana waliofanyiwa utafiti walikuwa na tatizo la nguvu za kiume. Wastani wa umri wao ulikuwa miaka 27.



Muhoozi: Kagame mtu hatari

MKUU wa Majeshi ya Uganda, Jenerali Muhoozi Kainerugaba, amezua mjadala mkali baada ya kuchapisha ujumbe kwenye mtandao wa kijamii wa X unaomlenga Rais wa Rwanda, Paul Kagame, akimwelezea kuwa “Mtutsi hatari zaidi kuwahi kukutana naye maishani.”

Kauli hiyo imeibua tafsiri tofauti kuhusu uhusiano kati ya viongozi hao wawili, baadhi wakiitafsiri kama dokezo kwamba Rais Kagame ni mtu mwenye historia ya kutumia nguvu kali dhidi ya wapinzani wake.

Ujumbe huu wa Jenerali Muhoozi, ambaye pia ni mtoto wa Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, umeongeza maswali kuhusu uhusiano wa kisiasa na kiusalama kati ya Uganda na Rwanda.



Trump kwenye sarafu ya USD

PICHA ya Rais wa Marekani, Donald Trump, imewekwa kwenye sarafu ya dola moja, ikiwa ni mara ya kwanza kwa picha ya rais aliye hai kuonekana kwenye fedha ya Marekani katika kipindi cha zaidi ya miaka 100.

Shirika la Uchapishaji wa Fedha la Marekani (U.S. Mint) limesema sarafu hiyo imetolewa kuadhimisha miaka 250 ya uhuru wa taifa hilo.

Jumatano iliyopita, Kampuni ya Marekani ya Mint ilizindua sarafu ya ukumbusho ya dola moja yenye picha ya Trump na kauli mbiu; “Tunamwamini Mungu”, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 250 ya Marekani.

Afrika ‘mpya’ yaidhinishwa UN

BARAZA Kuu la Umoja wa Mataifa limeidhinisha kubadilishwa kwa ramani ya kawaida ya dunia na kuweka nyingine inayoonyesha ukubwa halisi wa bara la Afrika.

Hii iliyopo inarekebisha ramani ya Merchanter iliyotengenezwa 1569 ikionyesha Afrika ina ukubwa sawa na Greenland, wakati ukweli inaizidi mara 14.

Azimio hilo lenye lengo la “Kurekebisha Ramani,” liliwasilishwa na Togo na kuungwa mkono na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika (AU), lilipitishwa kwa uungwaji mkono wa mataifa 164, yakiwemo Ufaransa na Uingereza.

Marekani ndiyo nchi pekee iliyopiga kura ya kupinga, huku nchi sita zikijizuia kupiga kura. Ingawa kura hiyo ya UN haina nguvu ya kisheria ya kulazimisha utekelezaji, itasababisha mabadiliko katika ramani zinazotumiwa na taasisi mbalimbali duniani kote.

Na Mzee TAI



Jicho la Tai

Uhamisho wa magavana siyo sabuni ya makosa yao

RAIS Samia Suluhu Hassan alipowaapisha wakuu wa mikoa na makatibu tawala wapya Ikulu Ndogo ya Tunguu, Zanzibar, Septemba 2, 2026, alitoa kauli iliyostahili kusikilizwa na kutafsiriwa mara mbili.

Alisema wakuu wa mikoa ni “jeshi lake,” na kwamba baadhi ya waliohamishwa walikuwa wakilalamikiwa kwa makosa ya kiutendaji na pengine yanayohusu ukiukwaji wa masuala kadhaa ya dhamana zao. Badala ya kuwaondoa, aliwapa nafasi nyingine ya kujirekebisha na hapa ndipo naiona huruma ya mama.

Hata hivyo, kwangu mimi, huruma hii ni nje-ma, lakini maswali hayana huruma. Kwa makosa madogo ya kiutendaji, uhamisho unaweza kuwa nafasi ya kuanza upya.

Kiongozi anaweza kukosea, kujifunza na kubadilika. Hata hivyo, pale taarifa zinazomfikia rais zikihusu tabia zisizofaa, kuingilia majukumu yasiyomhusu au tuhuma nzito, kuhamisha kituo pekee hakumalizi tatizo.

Ni kama kuhamisha pipa linalovuja kuto-ka sebuleni kwenda jikoni, halafu tukatangaza nyumba imekuwa safi.

Mkoa mpya siyo mashine ya kuosha rekodi, na mwenye tabia mbaya haachi, hasa anapokuwa na umri ulioenda kama hawa magavana wetu.

Ni kwamba wananchi wa Manyara, Lindi, Simiyu, Songwe au Morogoro hawapaswi kuwa maabara ya kupima kama kiongozi aliyelalamikiwa kwingine amebadilika.

Nao wanastahili uongozi bora tangu siku ya kwanza, siyo kusubiri mhesimiwa anayevurunda mahali ili wampokee.

Kama malalamiko yalikuwa ya kawaida, serikali ieleze hivyo. Kama yalihusu uzembe mkubwa, matumizi mabaya ya madaraka, kukosa uadilifu au jambo linaloweza kuwa la jinai, yafanyiwe uchunguzi wa haki na wa wazi.

Atakayebainika hana kosa asafishwe jina. Atakayethibitika kukiuka maadili awajibishwe. Na kama kuna ushahidi wa kosa la jinai, vyombo husika vifanye kazi bila kuangalia cheo.

Uhamisho usigeuzwe pazia la kuficha moshi. Natambua kuwa Rais Samia ana mam-laka ya kupanga safu yake na anaweza kuona uhamisho kuwa njia ya kuongeza ufanisi, lakini uongozi wa umma haupaswi kujenga dhana kwamba cheo ni koti linalohamishwa kutoka kabati moja kwenda jingine, hata likiwa na doa.

Uwajibikaji huimarisha taasisi; huruma isiyo na mipaka huzidhoofisha.

Tanzania haijakosa watu waadilifu, wenye elimu, uzoefu na uwezo wa kusimamia mikoa. Wengi wao hawajawahi kupata nafasi, siyo kwa sababu hawawezi, bali kwa sababu milango huzunguka majina yaleyale.

Kwa nini nafasi ya pili, ya tatu au ya nne apewe anayelalamikiwa, wakati kuna mwingine anayeweza kuanza akiwa na mikono safi na ari mpya? Kiongozi anapopewa nafasi mpya, wananchi wanapaswa kujua amepimwa kwa vigezo gani.

Serikali iweke utaratibu wa kutathmini utendaji wa wakuu wa mikoa kwa matokeo yanayoonekana; huduma, usalama, usafi, miradi, nidhamu ya fedha na namna wanavyowasikiliza wananchi.

Kamwe uteuzi usiwe tu jambo la kuamini moyo wa mteuaji; ujengwe pia juu ya taarifa zinazoweza kupimwa. Zaidi ya yote, utumishi wa umma siyo shule yenye mitihani ya marudio isiyoisha. Kila uamuzi una gharama kwa wananchi, miradi na imani ya taifa. Anayepewa dhamana lazima ajue kuwa kushindwa kuna matokeo, siyo tiketi ya kwenda mkoa mwingine. Kwa hiyo, naiheshimu huruma ya Rais Samia, lakini tunakumbusha kuwa huruma kwa kiongozi isimame sambamba na haki kwa wananchi. Aliyechemsha kidogo aonywe.

Aliyeshindwa kabisa aondolewe. Anayetuhumiwa achunguzwe. Uhamisho pekee usiwe msamaha wa kimyakimya na ninaamini kuwa taifa haliwezi kuendelea kubadilisha anwani za matatizo na kudhani limebadilisha tabia za watu. Ends

■ Habari Kuu

Lissu 'ahutubia' taifa kutoka kizimbani



Na Mwandishi WETU

KATIKA kipindi ambacho viongozi wa vyama vya upinzani wanakabiliwa na mazingira magumu ya kufanya mikutano ya hadhara, Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, anaonekana kujenga aina mpya ya jukwaa la kisiasa; kizimba cha Mahakama Kuu.

Lissu amekuwa mahabusu kwa zaidi ya mwaka mmoja akisubiri na kushiriki katika mchakato wa kusikilizwa kwa kesi ya uhaini inayomkabili, lakini, kinyume na matarajio kwamba kuwa mahabusu kungepunguza uwezo wake wa kuwasiliana na umma, kinachotokea ni tofauti.

Kila anapofikishwa Mahakama Kuu, Kanda

ya Dar es Salaam, kwa ajili ya kesi yake, Lissu amekuwa akitumia nafasi hiyo kutoa ujumbe mfupi kwa umma, aidha kabla kesi haijaanza au baada ya kesi kuahirishwa.

Ujumbe huo mara nyingi hubeba sekunde chache tu, lakini baada ya kurekodiwa na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii, hufikia hadhira kubwa zaidi kuliko ambavyo angeweza kufikia akiwa katika mazingira ya kawaida ya kisiasa.

Anapoingia katika chumba cha kusikiliza kesi, Lissu haonekani tu kuwa mshtakiwa anayefika mahakamani kusikiliza kesi, kizimba kimeanza kuwa sehemu ya mawasiliano yake ya kisiasa.

Katika mazingira ambayo mikutano ya hadhara imekuwa changamoto kwa baadhi ya viongozi wa upinzani, mahakama inampa Lissu nafasi ya kuonekana hadharani, hata kama kwa muda mfupi na katika mazingira yaliyowekewa mipaka na taratibu za mahakama.

Ujumbe wake hauishii ndani ya jengo la mahakama.

Unachukuliwa kwa simu, unawekwa kwenye mitandao ya kijamii, unasambazwa na wafuasi, wachambuzi na watumiaji wengine wa mitandao, na hatimaye kufika kwa maelfu au hata mamilioni ya watu ndani na nje ya Tanzania.

Kwa maana hiyo, kuta za mahabusu hazijawa kizuizi cha ujumbe wake; badala yake, kizimba cha mahakama kimekuwa sehemu ya kuufanya ujumbe wa Lissu kuvutia zaidi.

Kwa kawaida mwanasiasa anahitaji jukwaa, kipaza sauti na watu ili kuzungumza na wafuasi na wapenzi wake. Leo, simu moja inageuza sekunde 30 za maneno ya Lissu kuwa ujumbe unaosafiri duniani ndani ya muda mfupi.

Lissu mwenyewe anaonekana kutumia mazingira hayo kwa ufanisi kwani kila anapofikishwa mahakamani hakosi kusema jambo fulani.

Mwonekano wa Lissu

Zaidi ya maneno, Lissu pia analitumia jukwaa la mahakama kimuonekano kufikisha ujumbe mwingine kwa umma.

Lissu ‘ahutubia’

Inatoka Uk. 6

Kwa muda sasa, ameacha kunyoa nywele ambazo zimeanza kujisokota rasta, hilo nalo amelitolea ufafanuzi, akiwabeza wale waliokipachika chama chake jila la “chama cha marasta” kutokana na mwonekano wa mwenyekiti wake.

Kwa maneno mengine, mahabusu haijamnyamazisha kabisa Lissu; imebadili tu namna anavyowasiliana.

Ujumbe kwa wafuasi, wananchi

Pambazuko limefanya tathmini na kupata ujumbe mbalimbali ambao Lissu amekuwa akiutoa kutoka mahakamani.

Kwa kawaida hutoa maneno hayo kabla au baada ya usikilizwaji wa kesi hiyo, wakati huo, anapata fursa, ingawa finyu - ya kuwasiliana na watu mbalimbali waliomo mahakamani na kutoa kauli ambazo zinanaswa na kamera za simu za waandishi na wafuasi wa Chadema wanaofuatilia kesi hiyo kwani wakati huo wanakuwa huru kutumia simu zao.

Moja kati ya ujumbe uliosambaa sana wiki iliyopita ni ufafanuzi wake kuhusiana na rasta zake.

Baada ya Lissu kuacha kunyoa nywele ambazo zimeanza kujisokota rasta, baadhi ya wanaCCM walikipachika jina Chadema kuwa chama cha marasta.

Aliposikia hayo, Lissu akaamua kuwajibu; “Marasta ni wapigania uhuru. Rastas ni freedom fighters (wapigania uhuru). Waambie wamsikilize Bob (Marley) watajua kwa nini nina rasta,” alisema Lissu.

Bob Marley ni mmoja wa wanamuziki nguli wa Reggae duniani kutoka nchini Jamaica. Nyimbo zake nyingi zinabeba ujumbe wa ukombozi na utetezi kwa wanyonge.

“Na wasome historia na Mau Mau. Tunafuata nyayo za Dedan Kimathi, nyayo za mashujaa, sio wanaopokea vipande 30 vya fedha,” aliongeza Lissu wakati akikusanya makabrasha yake baada ya kesi kuahirishwa na kupigiwa kofi na wafuasi wake. Kimathi ni mpigania uhuru wa Kenya.



Awapongeza waandishi

Katika moja ya ujumbe ambao amewahi kuutoa kupitia jukwaa hilo jipya ni pongezi kwa waandishi na vyombo vya habari ambavyo vinaifuatilia na kuiripoti kesi hiyo.

Lissu, kabla kesi haijaanza kusikilizwa huku akicheka alisema; “ninafurahi sana ninapowana watu wa media (vyombo vya habari). Giza ni kitu kibaya, nchi inakufa kukiwa na giza. Vyombo vya habari mnafanya kazi nzuri,” alisema Lissu huku akiendelea kukusanya mafaili yake ya utetezi.

‘Anawamiss’ Watanzania

“Mmewaambia ninavyowamiss? Eee! Mmewaambia Watanzania ninavyowamiss?” alihoji Lissu siku nyingine na kujibiwa na wafuasi wake waliokuwa karibu; “Ndio, tumewaambia.”

“Waambieni si muda mrefu I will be back (nitakuwa nimerejea),” akasisitiza.

Huu ni moja ya ujumbe ambao ulisambaa sana kwa mujibu wa takwimu za utendaji za ukurasa wa Instagram wa Pambazuko.

Kauli za kisiasa

Lissu pia amekuwa akitumia jukwaa hilo kutoa kauli za kisiasa, akijibu baadhi ya kauli zinazotolewa na baadhi ya watu.

Inaendelea Uk. 8

■ Habari Kuu



Lissu ‘ahutubia’

Inatoka Uk. 7

Wiki iliyopita, alipoambiwa kuwa wapo watu wanamshutumu Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche, kuwa ndiye anayesababisha yeye ‘asote’ mahabusu kwani anakataa kufanya maridhiano jambo ambalo lingewezesha kesi hiyo kufutwa.

Lissu akajibu; “ni nani hao wanaosema hivyo? Ujinga huo wa hao wapokea pesa za Lumumba na ukome. Tunapigania haki, na kwa sababu tunapigania haki tupo tayari. Mimi nipo tayari kulipa kwa gharama yoyote. Waache ujinga.”

Kisha akaongeza; “sijawahi kuwaona mahakamani hata siku moja hao wanaonisemea. Kama wanataka kuniunga mkono waje mahakamani.”

Achomekea utani

Siku moja, akizungumza kama kawaida baa-da ya kesi kuahirishwa, Lissu aliwakaribisha wafuasi wake kumtembelea Ukonga anakoshikiliwa.

“Karibuni Ukonga,” alisema. Lissu alitoa ukaribisho huo huku akijua kuwa mamlaka zinawazuia watu wanaotaka kumtembelea, hata

mawakili anaowatumia kufanya utafiti katika kesi hiyo.

“Tunaruhusiwa kuja sasa?” Boniface Jacob, mmoja wa viongozi wa Chadema ambao wamekuwa wakiifuatilia kesi hiyo kwa karibu.

“Sijui. Mi nimesema karibuni,” alijibu Lissu huku akicheka kwa sauti. “Nyie mkipigwa mkwara kidogo tu mnanywea. Sio mnaniacha mie nadoda peke yangu huko,” akaongeza Lissu kwa bashasha.

Hata hivyo, Lissu akawaondoa wafuasi wake wasiwasi kwa kuwaeleza kuwa yuko vizuri na kuwa mambo hayo yataisha.

Pia akawahimiza wasiogope madhila ambayo wanayapitia sasa hivi na wafuatilie kwa karibu ujumbe uliomo katika nyimbo za Bob Marley.

Aonyesha ujasiri

Siku nyingine alitoa ujumbe kwa wafuasi wake akiwataka kutokuwa waoga, wakimuiga yeye ambaye licha ya kuwa gerezani kwa zaidi ya mwaka mmoja akikabiliwa na kesi ambayo hukumu yake ni kunyongwa hadi kufa, bado ni jasiri.

“Siku zote watu wenye hatia ndio huwa waoga. Watu wasiokuwa na hatia, sio waoga. Mimi sio mwoga kwa sababu sina hatia....”

“Na kwa sababu sina hatia, niko tayari kukaa gerezani as long as it takes (kwa muda wowote) ili kupigania haki,” alisema na kuongeza; “Bob Marley aliimba hivi; kweli inaweza kuwa kosa la jinai kwa watawala waovu lakini haijawahi kuwa dhambi.”

Apongeza mashahidi wake

Shahidi wake wa kwanza, John Mnyika, alipomaliza kutoa ushahidi, alimpongeza akimsifia kwa kazi mzuri aliyoifanya. Mnyika ni Katibu Mkuu wa Chadema.

Kisha akamwandaa Amani Golugwa, ambaye ni naibu katibu mkuu wa chama hicho, akimwambia kuwa yeye ndiye atakayefuata.

Naye siku alipokamilisha ushahidi wa kuongozwa, alimwagiwa maua na Lissu akimsifia kwa kazi anayoifanya.

Hata hivyo, Golugwa bado anaendelea kutoa ushahidi akijibu maswali ya dodoso kutoka kwa waendesha mashitaka.

Inaendelea Uk. 9

Lissu ‘ahutubia’

Inatoka Uk. 8

Kuteta na wafuasi

Lissu pia amekuwa akitumia wasaa mfupi baada ya kesi kuahirishwa kukutana na kuteta na wafuasi wake wakiwamo viongozi wa chama.

Alifanya hivyo wiki iliyopita alipoteta na kiongozi wa Bavicha wa chama chake baada ya kesi kuahirishwa.

Jukwaa hilo pia limegeuka fursa ya baadhi ya wafuasi wa Lissu nao kutoa maneno yao.

Pamoja na kauli za kisiasa lakini pia wapo ambao hutumia fursa hiyo kufanya maombi, wakimuomba kiongozi wao huyo afya njema na ujasiri wakati huu anapopitia kipindi cha majaribu.

Siku nyingine akapokea salamu kutoka kwa viongozi wa chama hicho mkoani Njombe ambao nao walikuja kusikiliza kesi.

Naye akatuma salamu kwa wana Chadema wa Njombe akisisitiza kuwa wachape kazi za chama kwani yeye yuko salama.

Kuhusu Nchimbi kufukuzwa

Siku chache baada ya aliyekuwa Makamu wa Rais, Dkt. John Nchimbi kufukuzwa uanachama wa CCM, Lissu alilizungumzia suala hilo kwa ujumbe mfupi;

“Watatoana maini,” alisema huku akita-basamu na kuonesha ishara ya dole gumba.

Lissu awapiku viongozi

Hatua ya Lissu kuzungumza na hadhira ndani ya Mahakama Kuu na nje ya viunga vya chombo hicho cha kusaka haki, anapata mwanya mpana zaidi kuwasiliana na umma zaidi ya viongozi wengine wa chama chake.

Hii inaleta kitendawili cha kisiasa kwani inaonekana kuwa mwanasiasa aliye katika mazingira yenye vikwazo zaidi ndiye anayepata nafasi ya kuzungumza na hadhira pana zaidi.

Mitandao ya kijamii nayo imekuwa kiungo muhimu katika mchakato huo. Ujumbe wa Lissu unapochukuliwa na kusambazwa, hauendi kama taarifa ya mahakamani pekee, unakuwa maudhui ya kisiasa yanayojadiliwa, kutaf-siriwa, kupingwa au kuungwa mkono na watumiaji wa mitandao.

Kwa mtazamo huo, Lissu anaweza kuwa anafanya zaidi ya kutoa ujumbe, anaendelea kujenga uwepo wake wa kisiasa.

Na huu ndio umuhimu wa kile kinachotokea kizimbani, ambako kimsingi mahakama ni eneo la kusikiliza mashauri ya kisheria, imekuwa pia mahali ambapo ujumbe wa kisiasa wa Lissu unatokea na kusafiri kwenda kwa umma.

Hata hivyo, Pambazuko halikuweza kubaini iwapo kama huu ni mkakati uliopangwa tangu mwanzo au ni matokeo ya mazingira yaliyomzunguka Lissu.

Lakini jambo moja ni dhahiri kuwa kesi inayomweka Lissu mahabusu pia inampa fursa ya kuendelea kuwa sehemu ya gumzo la kisiasa nchini.

Kwa hiyo, kila safari ya Lissu kwenda mahakamani haionekani tena kwa wafuasi wake kama safari ya kisheria pekee. Inakuwa pia fursa ya kupokea ujumbe kutoka kwa mwenyekiti.

Kwa Lissu, kizimba, badala ya kuwa mwisho wa sauti yake ya kisiasa, kimegeuka kuwa jukwaa dogo lenye hadhira kubwa.



Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

Jaji mkuu na mahakama zetu



MHESHIMIWA Jaji Mkuu George Masaju, kwa mara kadhaa ametoa maelekezo mbalimbali kwa watendaji wa mhimili wa mahakama na kwa umma mzima.

Siku chache zilizopita ametoa onyo kwamba “hawataruhusu watu kuidharau mahakama.”

Kwa heshima na unyenyekevu nampongeza kwa jitihada anazofanya, lakini namuomba sana apitie maoni yangu haya.

Wananchi wa kawaida hawawezi kuidharau mahakama kamwe. Watanzania hawa ninaowajua na yeye anawajua, wanaiheshimu na kuio-gopa mahakama.

Utitiri wa kesi na subira ya wananchi kusubiri haki inayocheleweshwa, ni ushahidi kuwa wananchi hawaidharau mahakama, bali wanaiheshimu hata bila uwepo wa sababu ya kufanya hivyo.

Tatizo walilo nalo wananchi ni imani ndogo kwa mhimili huo. Imani imeshuka sana na walio wengi ama wanajichukulia sheria mkononi au wanatafuta fedha kununua haki zao. Kutoiambi mahakama ni tofauti na kuidharau.

Mahakama zetu zinadharauliwa na makundi mawili yaani; serikali na watendaji wa mahakama. Serikali inaidharau mahakama ama kwa kuiingilia, kudharau uamuzi wake na kutolipa maslahi stahiki, na raslimali na nyenzo za kufanyia kazi.

Watendaji (majaji, mahakimu na watendakazi wengine) wanaweza ama wanaidharau au kuidharaulisha mahakama. Zaidi wanaweza kuwa wanafanya yote mawili kwa wakati mmoja.

Urasimu, umaskini, ujinga na “kujiona” (indispensability) kwa watumishi wa vyombo vya utoaji haki, ni baadhi ya vikwazo vinavyomomonyoa imani ya wananchi kwa mahakama.

Hapa nashauri Masaju asimame upande wa “wajinga” wanaolipa kodi inayoendesha mahakama badala ya matamshi yanayowalinda wanaowaringia wananchi.

Mara kadhaa Jaji Mkuu Masaju, labda bila kukusudia amelumbana na wana harakati wa haki za binadamu na utawala wa sheria, akielekea kuonyesha ubaya wa uanaharakati. Nina hakika, heshima na fahari ya mahakama mahali popote, hutokana na mahakama kuchukua msimamo imara wa kiharakati (judicial activism) katika kutetea ukuu wa katiba na sheria. Jaji mkuu wetu asiunee haya uanaharakati.

Katika mfumo ambamo mihimili ya mahakama na bunge imefanywa dhaifu mbele ya mhimili wa serikali, mahakama inalo jukumu zito la kutetea upekee na uhuru wake bila kujali madhara na gharama zake.

Wanaoitesa na kuibagaza mahakama huko serikalini ni wateja wa baadaye wa mahakama hiyo watakaotamani iwe huru na inayotenda haki.

Bila kulinganishwa na mhimili wowote, mahakama inalo jukumu “lisilo la kuagizwa” katika kulinda utakatifu, uhuru na weledi wa mahakama.

Kiongozi wa jukumu hili ni jaji mkuu. Namuomba Masaju asiwe na udhuru, asichoke, asio-gope kuitwa mwana harakati na asione aibu kutetea uhuru wa mahakama ambalo ni kimbilio la wanyonge wengi.

Jaji Masaju ajiepushe kutetea “kutokukosea” kwa mahakama na ashupalie uhuru wa mahakama na kamwe si uhuru wa mahakimu wala majaji.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Tanzania bado upo ujasiri wa kuuliza maswali?

KILA siku ninapoitazama nchi yetu na mambo yanayoibuka, ninawiwa kuuliza iwapo mimi na wenzangu wa nchi hii tumewahi kutulia na kujiuliza maswali.

Nilipomsikiliza Askofu Benson Bagonza akieleza jinsi ambavyo inaelekea ukweli hautakiwi katika nchi hii na pia rushwa imekosa askari wa kuishughulikia, nikahisi kuwa sisi wenye nchi tumeshindwa kutekeleza wajibu wetu tukiwa raia.

Katika demokrasia matarajio yaliyopo ni kuuliza maswali magumu, kujiuliza binafsi, hatimaye kuwahoji wenye dhamana ya kuongoza nchi ili kupata majibu na njia sahihi ya kurekebisha yanayoonekana kwenda mrama.

Siyo lazima kupata majibu, lakini kwa raia la muhimu ni uwezo tulionao na ujasiri wa kuuliza maswali magumu.

Kama taifa linalojiamini na lenye raia wanaojiamini, maswali ni lazima yaulizwe na kujiuliza na hii ni njia mojawapo ya kutafuta ukweli ambao utatuwezesha kusonga mbele kama taifa.

Tunaendelea kushuhudia mabadiliko na matukio yakiendelea hasa kwenye uwanja wa siasa na kuibua minong'ono kutoka kwa wananchi wa hali na rika mbalimbali.

Wapo waliosema, kwa nini hayo yametokea na wengine, kwa nini wakati huu na kulikoni? Je kuna mambo yanayofichwa kama raia hatujaambiwa.

Ili mradi yanawazwa mengi, nikamsikia mtu mwingine akisema, hivi katika nchi hii bado mnataka kuuliza maswali? Kwani raia bado tuna nafasi ya kuuliza maswali magumu bila kuonekana kuwa tunapinga uongozi wa nchi? Hili swali si dogo.

Ibara ya 3 ya Katiba inaitaja Tanzania kama nchi ya kidemokrasia na demokrasia huwa haizuki tu bali inajengwa.

Ili kuijenga demokrasia haiwezekani watu wote kuwa na mawazo yanayofanana. Ujenzi wa demokrasia ya kweli hutokana na uwezo wa watu kuwa na mawazo yanayotofautiana, kuhoji, kujadili na ikibidi kuweza kukosoa bila hofu.

Serikali ikikosolewa haiachi kuwa serikali inabaki

kuwa serikali na inapaswa kusikiliza. Hata vyama vya siasa vinaweza kuulizwa maswali na hata kukosolewa, hii haivibadilishi kuwa kitu kingine, navyo hubaki kuwa vyama vya siasa.

Inawezekana pia kiongozi akaulizwa swali kuhusu uamuzi alioufanya naye pia anapaswa kujibu na kutoa maelezo bila kudhani muuliza swali ana kisa naye.

Uzoefu wangu katika nchi hii, nimegundua mara nyingine, kama si mara nyingi, tunachanganya mambo haya; kukosoa na kuchukia, kuhoji na kupinga.

Hali kama hii inatupeleka katika kupoteza kitu muhimu sana katika demokrasia ambacho ni fursa ya mazungumzo.

Ikitokea raia akakutana na jambo asilolielewa anapaswa afanye nini? Je, ni sawa kunyamaza? Au inabidi aulize? Tukiwaangalia waandishi wa habari nao, wakikutana na jambo linalogusa maslahi ya umma, je waache kuuliza kwa kuwa wakiuliza huenda swali lao likamuudhi mtu mwenye mamlaka anayeulizwa?

Na kwa mtu kama mtetezi wa haki za binadamu, akiuangalia mfumo fulani unaoonekana kuweza kumduru mwananchi, je, wajibu wake ni kuwa kimya au kuinua sauti na kuuliza bila yeye kueleweka vibaya?

Ninavyoona mimi kuuliza inapobidi ni wajibu na si hiari. Nchi yetu haitaweza kujengwa kwa watu kuwa kimya kwa hofu ya kuuliza maswali.

Tufike mahali ambapo swali gumu liwe fursa na si tishio, mwananchi aweze kuuliza swali bila hofu, mwanahabari achunguze bila kutishiwa.

Mwishowe ijulikane wazi kuwa taifa kuulizwa maswali si udhaifu ni kujiamini. Kwa wiki hii tujiulize sote 'Bado tuna ujasiri wa kuuliza maswali?'

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwana-harakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.



■ Habari

Kigogo Udasa ahofu Katiba Mpya, aibua Tanganyika



Dkt. Dominicus
Makukula

Na Waandishi WETU

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam (Udasa), Dkt. Dominicus Makukula, haamini endapo Katiba Mpya itapatikana kabla ya mwaka 2030.

Akizungumza na Pambazuko katika mahojiano maalum ofisini kwake Dar es Salaam, wiki iliyopita, Dkt. Makukula amesema wasiwasi wake unatokana na kutokuwepo kwa maandalizi yoyote ya msingi na ya wazi hadi sasa kuhusu mchakato huo.

Mwanazuoni huyo amesema mchakato wa kupata Katiba Mpya - kwa kawaida, huchukua muda mrefu, hivyo kwa muda uliosalia kufika 2030, ni mfupi. Ni chini ya miaka minne kuanzia sasa.

Aidha, katibu huyo amesema katiba Mpya ya Tanzania inapaswa kutanguliwa na Katiba ya Tanganyika kwa sababu mbia mwingine wa Muungano; Zanzibar, tayari ana katiba yake.

Akifafanua, Dkt. Makukula amesema ili Muungano uonekane kuwa wa usawa, ni vyema kila mbia kuwa na nafasi sawa. Kwamba kwa kuwa Zanzibar ina Katiba yake, basi na Tanganyika nayo inapaswa kuwa na katiba yake.

“Ili Tanganyika na Zanzibar ziweze kuunga na vizuri, basi na Watanganyika lazima wadai vitu vyao vinavyowahusu ili pande mbili zita- kapoungana kila moja ijue inaleta nini mezani,” amefafanua. Ameshangaa wahusika wa kuan- daa mchakato wa Katiba Mpya kuwa na kigu- gumizi kuanza mchakato huo mapema licha ya wadau vikiwamo vyama vya siasa kudai suala hilo na kwamba Chama Cha Mapinduzi (CCM) imeahidi suala hilo ndani ya ilani yake.

“Ninashangaa wapi tunakwama, kwa sababu jambo lenyewe hilo la Katiba Mpya limeguswa tayari kwenye maeneo makubwa matatu...”

“Kwenye mashirika ya kiraia tayari huko in- aonekana ndiyo kama watu walikuwa wamean- za kuzungumza wao wenyewe, lakini ukifika kwenye ofisi ya serikali, yaani kwa maana ya rais, tayari rais ameshazungumzia suala hilo kwamba kutakuwa kuna mabadiliko ya katiba...”

“Lakini ukienda kwenye Ilani ya CCM, hilo limetajwa waziwazi, na hata ilani za vyama vingine vya siasa vyenyewe vilikuwa tayari vi- mekwishazungumzia mambo hayo...”

“Kama mnakumbuka mwaka jana, sisi tu- liendesha mdahalo wa vyama vya siasa ambavyo vilikuwa vinatarajia kwenda kushiriki uchaguzi mkuu wa udiwani, wabunge na rais...”

“Na juzi kwenye kongamano la Tanzania De- mocracy Forum lililoandaliwa na TLS (Chama cha Wanasheria Tanganyika), walikuwepo watu mashuhuri; kina mzee Warioba, Profesa Shivji, Rose Mwakitwange, James Mbatia, Profesa Ti- baijuka na wengine wengi, lakini sikuona uwak- ilishi wa kutosha kutoka kwenye chama tawa- la, nafikiri kulikuwa kuna baadhi ya wajumbe ila hawakuwa wale mashuhuri,” amesema Dkt. Makukula.

CCM: Tunaomba Mungu Polepole apatikane hai

Na Mwandishi WETU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kinaendelea kusikitishwa kutopatikana kwa Humphrey Polepole, aliyekuwa balozi wa Tanzania nchini Cuba.

Akizungumza katika mahojiano na Edwin Odemba wiki iliyopita, katibu wa halmashauri ya chama hicho – Itikadi, Mafunzo na Uenezi, Kenani Kihongozi amesema kuwa CCM inaendelea kufuatilia alipo Polepole na kuhimiza vyombo vya usalama kuongeza nguvu kumpata.


“CCM haitamani kuona hata mtu mmoja anapotea, tunaomba Mungu Polepole apatikane na vyombo vya usalama vinafanya kazi kubwa kufuatilia jambo hili,” amesema Kihongozi.

Kihongozi amesema CCM inaamini vyombo vya usalama vinaendelea kufanya uchunguzi wake kuhusu alipo Polepole na vikamilisha kazi zake, vitaeleza nini kilitokea na pengine kueleza alipo kada huyo.

Polepole aliyewahi pia kuwa katibu wa itikadi na uenezi wa chama hicho tawala alitekwa na watu wasiojulikana akiwa maeneo ya Un-unio, Dar es Salaam alfajiri ya Oktoba 6, 2025.

Familia yake ilisema watu wasiojulikana walivamia nyumba hiyo na kumchukua kwa nguvu, milango ilikutwa imevunjwa, nyaya za umeme zimekatwa na damu ikiwa ndani na nje ya nyumba. Polisi walitangaza uchunguzi, lakini hadi sasa hakuna taarifa ya wazi kuhusu alipo wala waliomchukua.

Kesho yake, mawakili wake waliwasilisha maombi ya habeas corpus Mahakama Kuu, wakitaka mamlaka zimfikishe mahakamani. Maombi hayo yalitupiliwa mbali Oktoba 24, mwaka jana baada ya mahakama kusema haku-na ushahidi uliothibitisha kwamba taasisi za serikali zilihusika na kutoweka kwake.



Uamuzi huo haukujibu hadharani swali la msingi; Polepole yuko wapi hadi leo?

Kihongosi amesema CCM inaamini uchunguzi unaendelea na kwamba vyombo husika vitatoa maelezo baada ya kukamilisha kazi yake.

Hata hivyo, msimamo huo unakabiliwa na shinikizo la wanaharakati wanaotaka majibu ya haraka na uwajibikaji.

Tigere Chagutah wa Amnesty International amesema kutoweka kwa Polepole kunatia hofu, akiitaka serikali kuweka nguvu zote kumpata, kuhakikisha usalama wake na kuwafikisha wahusika mbele ya sheria.

Mwanaharakati Maria Sarungi Tsehai amesema tukio hilo lilivuka “mstari mwingine mwekundu,” huku Human Rights Watch ikilitaja kuwa jambo la kutisha na kutaka mamlaka ziache kuzima sauti za ukosoaji.

Wanaharakati na watu wengi bado wanahitaji kujua yuko wapi mwanasiasa huyo ambaye baada ya kuamua kuondoka kwenye utumishi wa serikali na kuachia dhamana ya ubalozi, alikuwa “mwiba” kwa watawala akiwatuhumu kwa masuala kadhaa makubwa yakiwamo ya rushwa, uonevu na uvunjifu wa katiba.

“Ikiwa Polepole anashikiliwa kwa tuhuma yoyote, Katiba na sheria vinataka afikishwe mahakamani, ikiwa alitekwa na watu binafsi, serikali ina wajibu wa kuwatafuta na kumrudisha salama,” amesema Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika, Boniface Mwabukusi.

Mwabukusi amekuwa akieleza kuwa CCM, ikiwa chama tawala na taasisi aliyowahi kuitumikia, ina wajibu mkubwa kuhakikisha Polepole anapatikana akiwa hai, kuliko kueleza masikitiko.

Habari

Pambazuko laripoti, Samia akerwa uchafu Dar



Na Elizabeth HOMBO

MIEZI michache baada ya gazeti hili kuandika habari za uchunguzi kuhusu uchafu na ubovu wa mifereji ya majitaka inavyohatarisha afya za watu, hatimaye Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha kukerwa na hali hiyo katika Jiji la Dar es Salaam.

Mbali na Rais Samia, Spika wa Bunge, Mussa Zungu, naye alizungumzia suala hilo la uchafu katika jiji hilo kubwa la kibiashara nchini, akiwaonya watendaji wa Tamisemi kwa mwenendo usioridhisha unaoshindwa kuwabana watu kutunza usafi wa mazingira.

Onyo la Rais Samia

Akizungumza wiki iliyopita wakati akiwaapisha viongozi wateule Ikulu Ndogo ya Tunguu, Zanzibar, Rais Samia alilizungumzia suala hilo licha ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, kuto-kuwepo kwenye hafla hiyo.

Katika suala hilo, Rais Samia alisisitiza umuhimu wa kusafisha mitaro na kuondoa taka zinazozuia mtiririko wa maji.

Mkuu huyo wa nchi, akaelezea namna baadhi ya mitaro ilivyojaa uchafu huku ikizibwa na marundo ya viroba vya taka ngumu, hali inayosababisha kuziba na kuzuia maji kupita.

Alitoa kauli hiyo wakati akisisitiza umuhimu wa mamlaka mbalimbali kufanya maandalizi ya kukabiliana na madhara ya mvua kubwa za el nino zinazotabiriwa kuanza kunyesha mwishoni mwa mwezi huu katika mikoa kadhaa nchini.

Watalaamu wameshaeleza kuwa mvua hizo zinaweza kusababisha mafuriko katika maeneo kadhaa nchini hivyo serikali imezitaka mamlaka katika ngazi mbalimbali kuhakikisha maandalizi yanafanyika kukabiliana na madhara ya hali hiyo.

Katika hotuba yake, Rais Samia alisema wananchi pia wana mchango katika tatizo hilo kwa kutupa taka kwenye mitaro, hivyo amewataka kubadili tabia na kushirikiana katika kuweka mazingira safi.

Rais Samia pia alieleza kusikitishwa kwake na hali ya usafi katika baadhi ya miji nchini, hususan Dar es Salaam, akisema haipendezi kuona taka zikiwa mitaani.

Makala ya Pambazuko

Makala ya uchunguzi kuhusu uchafu wa mazingira, ilichapwa na gazeti hili Machi 23, 2026, ambayo ilijikita zaidi katika eneo la Mwenge, Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Gazeti hili katika uchunguzi wake wa takribani miezi mitatu iliwahoji wananchi wa eneo hilo la Mwenge, ambapo walieleza wasiwasi wao wa kukumbwa na magonjwa ya kuambukizwa kutokana na ubovu mkubwa wa mfumo wa maji taka.

Mrundikano wa taka katika mitaro unasababisha mifumo ya majitaka kupasuka mara kwa mara na kusababisha athari kubwa kiafya na katika mazingira.

Gazeti hili pia ilichunguza na kubaini kuwa miundombinu ya maji taka katika eneo la Mwenge ilijengwa zaidi ya miaka 50 iliyopita na bado haijawahi kufanyiwa ukarabati mkubwa, kupanuliwa au kuwekewa mifumo mipya.

Gazeti hili pia ilibaini kuwa tatizo hilo la kupasuka mara kwa mara kwa mashimo ya maji taka, lina- tokana na miundombinu kuzidiwa kutokana na idadi ya watu kuongezeka.

Makala hiyo ni moja ya makala bora zilizoteuliwa kwa ajili ya Tuzo za Samia Kalamu Awards na sasa iko kwenye hatua ya kupigiwa kura kupitia kiunganishi hiki;

<https://samiaawards.tz/mshiriki/260251>

Wafanyakazi IPTL waiangukia serikali iwalipe

Mwandishi WETU

BAADHI ya waliokuwa wafanyakazi wa kampuni ya kufua umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), wameiomba serikali iharakishe malipo ya stahiki zao ili waweze kutafuta makazi mapya.

Wafanyakazi hao wameomba hivyo baada ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, kubariki kuondolewa kwao kwenye nyumba za kampuni hiyo.

Wameliambia Gazeti la Pambazuko kuwa kwa sasa hawana mahali pa kuishi wao na familia zao wakiwamo watoto, hivyo wanaiomba serikali kupitia Hazina iharakishe kuwalipa stahiki zao ambazo wanaidai kampuni hiyo ambayo kwa sasa ipo chini ya serikali baada ya mgogoro uliokuwepo kati yake na mmiliki, Harbinder Sing Sethi, kuamuliwa na Mahakama Kuu.

Wafanyakazi hao ni waliokuwa wameombwa na uongozi wa kampuni ya IPTL kulinda mitambo, magari pamoja na nyumba kadhaa zilizokuwa makazi ya maofisa wa kiwanda na walipewa mikataba ya kuendelea kuishi hapo hadi watakapokuwa wamelipwa stahiki zao Hazina.

Mmoja wa wafanyakazi hao, Willbroad William, amesema wameshangazwa na kauli ya mkuu huyo wa wilaya, Mtambule, kuwaamuru waondoke bila kujali kuwa wako na familia, lakini kikubwa bado wanaidai serikali stahiki zao.

Wafanyakazi hao wamesema baada ya kampuni hiyo kufungwa, waliokuwa wakurugenzi; Ambroce Brixson Lugenge kwa niaba ya mwenyekiti (Seth) na Joseph Makandeghe (mwana sheria) waliwakabidhi nyumba hizo na mali zingine kwa mkataba maalum kwamba waendeleo kuzilinda wakati wanasubiri malipo yao.

Akizungumza kwa sharti la kutotajwa jina lake, mfanyakazi mwingine amesema baada ya



Vifaa vya ndani vikiwa vimetupwa nje ya nyumba za IPTL zilizoko Salasala, Dar es Salaam kama vilivyokutwa juzi. Na Mpigapicha Wetu.

kiwanda cha IPTL kufungwa na serikali na badaye aliyekuwa mmiliki wake, Sethi, kuwekwa rumande, waliokuwa wakurugenzi wa kampuni hiyo waliwapa barua za kuwaondoa kazini zikiambatana na madai na stahiki za kila mfanyakazi.

“Leo (Jumamosi Septemba 5, 2026) Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni amekuja hapa na kuumuru tuondoke, akisema hizi nyumba ni mali ya Sethi, kwa kuwa sisi hatuna cha kufanya, tunaomba serikali kupitia Hazina watulipe mafao yetu...”

“Hapa tunapoongea tumefungiwa nje ya geti, haturuhusiwi kuonekana kwenye eneo hili, tunaamini Rais Samia Suluhu Hassan asingependa kuona tunanyanyasika kiasi hiki, tunamuomba asikie kilio chetu, watulipe ili tutafute mahali pa kujistiri na familia zetu, hata fedha za kuhamisha mizigo yetu hatuna,” amesema mmoja wa wafanyakazi hao

Akaongeza; “Kwa sasa tupo tunahangaika kuhamisha familia zetu, hatujui hata tunaelekea wapi, tangu awali sisi hatukuwa wakaidi kuondoka kwenye hizi nyumba, bali tulikuwepo kwa sababu hatujalipwa fedha zetu ambazo tunadai kwa mujibu wa sheria.”

Akizungumza na wafanyakazi hao, Jumamosi Septemba 5, 2026 Mtambule aliwataka wafanyakazi hao ambao alidai kuwa ni walinzi waliokuwa wanaishi katika nyumba za IPTL zipatazo 12 kuondoka mara moja.

■ Habari

Matumaini matibabu selimundu yapatikana



Dkt. Mouhamadou Sow akionyesha dawa iliyogunduliwa na Maabara ya Teranga kwa ajili ya ugonjwa wa Selimundu huko Senegal.

Na Mwandishi MAALUM

KILA siku Rahma Abdallah hulazimika kufikiria jambo moja muhimu kabla ya mambo mengine; 'dawa yake'.

Rahma, ambaye anaishi Chanika, Dar es Salaam, ni mmoja wa watu wanaoishi na ugonjwa wa selimundu (sickle cell) ambao humlazimisha mgonjwa kuishi kwa kutegemea dawa ya 'hydroxyurea' kusakaidia kudhibiti athari za ugonjwa huo.

Kwa siku analazimika kutumia vidonge viwili vya dawa hiyo, ambapo kila kidonge hununua kwa Shilingi 2,000.

"Ni changamoto sana, hasa unapokuwa huna kazi na unategemea ndugu," anasema katika mahojiano ya Pambazuko.

Kwa wagonjwa wengi wa selimundu, hydroxyurea siyo dawa ya kawaida tu, inaweza kuwa sehemu muhimu ya maisha yao, hususan kusakaidia kupunguza baadhi ya madhara na vipindi vya maumivu makali vinavyoweza kujirudia.

Ndiyo maana taarifa za Senegal kuanza uzalishaji wa dawa hiyo zimepokelewa kwa matumaini mapya miongoni mwa baadhi ya watu wanaoishi na ugonjwa huo na wadau wa afya Afrika.

Dawa hiyo, inayofahamika kwa jina la kitaalamu Drepaf, inayozalishwa nchini Senegal na kampuni ya dawa ya Teranga Pharma, kwa ushirikiano na taasisi ya Drep Afrique. Dawa hiyo ni ainasafu (generic) ya hydroxyurea.

"Senegal kuanza utengenezaji wa dawa za selimundu ni hatua nzuri, kwa sababu bei ya dawa inaweza ikashuka na zinaweza kupatikana kwa wingi," anasema Rahma.

Matumaini kwa Afrika

Daktari Collin Kanza kutoka Kituo cha Matibabu ya Selimundu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, anasema hatua iliyofikiwa na Senegal ni mafanikio makubwa kwa mapambano dhidi ya ugonjwa huo barani Afrika.

"Ni hatua kubwa sana. Senegal ina wagonjwa wachache wa selimundu ikilinganishwa na baadhi ya nchi nyingine za Afrika, lakini imeweza kufanya jambo hili kubwa..."

"Sisi Tanzania tuna uhitaji mkubwa zaidi wa dawa hizi. Ni wazi tunalo la kujifunza na kuiga mfano kutoka kwao," anasema Dkt. Kanza.

Tanzania inashika nafasi ya nne duniani na ya tatu Afrika kwa idadi kubwa ya wagonjwa wa selimundu, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Takwimu za Wizara ya Afya zinaeleza kila mwaka kuna watoto 11,000 hadi 14,000 wanaozaliwa na ugonjwa huo nchini Tanzania.

Matibabu ya ugonjwa huu wa kurithi ni ya muda mrefu, hivyo, kupatikana kwa dawa kwa urahisi na kwa gharama nafuu kunaweza kuleta tofauti kubwa katika maisha ya wagonjwa na familia zao.

Inaendelea Uk. 17

Matumaini matibabu

Inatoka Uk. 16

Hatua ya Senegal pia inafungua mjadala mpana kuhusu uwezo wa Afrika kuwekeza katika uzalishaji wa dawa muhimu zinazohitajika kwa watu wake.

Kwa sasa baadhi ya dawa zinazotumiwa na wagonjwa wa selimundu nchini zinapatikana kupitia uzalishaji na mifumo ya usambazaji kutoka nje ya Afrika, ikiwamo hii ya hydroxyurea.

Iwapo uzalishaji wa hydroxyurea utaongezeka barani Afrika na dawa hiyo kusambazwa katika nchi nyingine, matumaini ya wagonjwa wengi ni kwamba gharama inaweza kushuka na upatikanaji wake kuongezeka.

Bima ya afya

Wizara ya Afya iliingiza dawa hii katika orodha ya dawa zinazopatikana ndani ya bima ya afya.

Kwa Felister John, mzazi wa shujaa wa selimundu anayeishi Kigoma, kuwa na bima ya afya kwa mtoto wake kumeleta mabadiliko makubwa. Anasema kabla ya bima hiyo familia yake ilipitia changamoto kubwa kwa sababu alilazimika kutoa fedha nyingi kutoka mfukoni kununua dawa na gharama nyingine za matibabu.

Hata hivyo, kwa familia ambazo hazina uwezo wa kugharamia bima, mzigo wa matibabu ya selimundu unaweza kuwa mkubwa zaidi.

Julieth Mombuli ni miongoni mwa wale wanaopambana kila siku kuhakikisha mtoto wake anapata dawa.

“Mimi ndiye baba na mimi ndiye mama, baba yake alikataa kwamba huyu si mtoto wake, nilimpata kwa mwanaume mwingine nje ya ndoa, jambo ambalo si la kweli...”

“Hivyo, sina jinsi ya kufanya. Naumia, lakini ni mwanangu siwezi kumuacha akiteseka peke yake. Ninafanya biashara ndogondogo, kuna wakati nalazimika kujinyima ili angalau mwanangu apate dawa,” anasimulia kwa uchungu.

Anasema mwanawe anapotumia dawa ya hydroxyurea hupata nafuu kubwa, humsaidia kupunguza vipindi vya maumivu makali vina-vojirudia mara kwa mara.

Kwa Julieth, kutafuta fedha za dawa ni sehemu ya mapambano ya kila siku ya kumlea mtoto anayeishi na selimundu.

Mahitaji ni makubwa

Veronica Mrema, Ofisa Habari wa Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Selimundu Tanzania (SCDPCT), anasema jumuiya hiyo imekuwa ikisaidia baadhi ya watoto wanaoishi na ugonjwa huo kupata bima ya afya.

“Mahitaji bado ni makubwa. Ila tangu Januari mwaka huu hadi sasa, tumeweza kuwakatia bima ya afya watoto 36 tu kwa kushirikiana na mdau mmoja aliyetuunga mkono.

“Orodha tuliyonayo bado tuna wengine wengi ambao hatujaweza kuwafikia kwa sababu uhitaji ni mkubwa, tuna wagonjwa zaidi ya 300 na asilimia kubwa ni wahitaji,” anasema.


Anasema kwa muktadha huo, hatua ya Senegal kuanza uzalishaji wa hydroxyurea ni hatua inayostahili pongezi kubwa na ina maana kubwa katika mapambano dhidi ya selimundu.

“Kwa hatua ambayo Senegal imeweza ku-fikia, imetuletea faraja kubwa. Ni hatua kubwa, na mashujaa, wazazi na walezi wameipokea kwa furaha kubwa,” anasema.

Bei itashuka?

Watu wanaoishi na selimundu nchini wana matumaini kwamba iwapo Senegal itafikia uwezo wa kuzalisha dawa kwa kiwango cha kutosheleza na kuisambaza katika nchi nyingine za Afrika, ikiwamo Tanzania, gharama za ununuzi zinaweza kupungua kwa kiasi kikubwa.

Kwa Rahma, ambaye kwa sasa hununua vi-donge viwili kwa siku, matumaini hayo yana maana kubwa.





Mradi wa LNG watikisa dunia



Na Mwandishi WETU

HAUJAANZA rasmi lakini mradi wa kuchakata gesi asilia (LNG) ambao umepangwa kujengwa Lindi, Tanzania, unaitikisa dunia.

Habari zilizochapishwa hivi karibuni zimeuorodhesha mradi huo miongoni mwa miradi mikubwa sana duniani ambayo inaangaliwa na kufuatiliwa kwa karibu zaidi na China, Ulaya na Marekani.

Mradi huo wa kuchakata LNG nchini Tanzania unakadiriwa kugharimu dola za Marekani bilioni 42 (zaidi ya Shilingi trililioni 105).

Miradi mingine mikubwa ni pamoja na mradi wa kusafisha mafuta ghafi wenye thamani ya dola bilioni 17 Nigeria, ikiwa ni uwekezaji wa tajiri namba moja Afrika, Aliko Dangote, na mradi wa bomba la gesi kati ya Nigeria na Morocco wenye thamani ya dola za Marekani bilioni 25. Mwingine ni ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege nchini Ethiopia.

Wachambuzi wa masuala ya uchumi na uwekezaji wanaeleza kuwa miradi hiyo italeta mabadiliko makubwa siyo tu Afrika, bali duniani katika nyanja za nishati, usafiri wa anga, michezo na kuiweka Afrika kama mshindani katika ngazi ya dunia.

Moja kati ya mambo makubwa yanayoangaliwa kupitia miradi hii ni uwezo wake wa ku-geuza uwekezaji kuwa ajira za kudumu, kuinua uchumi na kupanua biashara za kikanda.

Kwa upande mwingine, wachambuzi wanasubiri kuona iwapo miradi hiyo inaweza kuli-komboa bara la Afrika kutoka kwenye matatizo yake sugu ikiwemo ukosefu wa nishati na gharama kubwa za usafiri na usafirishaji kwa kutegemea mafuta yanayoagizwa nje ya bara hilo.

Wachumi wanaamini kuwa iwapo miradi hiyo itatekelezwa kwa weledi, ina uwezo mkubwa wa kuleta mapinduzi katika nyanja nyingi ikiwemo nishati, usafiri wa anga, biashara na mnyororo wa madini.

Akiba ya gesi Tanzania

Mradi huo unatajwa kwamba utakuwa chanzo cha kuvutia wawekezaji wa kimataifa kutokana na Tanzania kuwa na akiba kubwa ya gesi asilia ambayo tayari imeshagunduliwa.

Siku za hivi karibuni mradi huo umeanza kuwaamsha wawekezaji, hasa baada ya vita vya Marekani na Iran, vinavyosababisha kufungwa kwa lango la Hormuz, ambalo hutumika kupitisha sehemu kubwa ya mafuta yanayotoka nchi za Ghuba. Mradi huo wa LNG unaonekana sasa kuwa kama mbadala wa utegemezi wa mafuta na hivyo kushika macho ya wawekezaji wakubwa duniani katika eneo la nishati.

Usafishaji mafuta

Tajiri namba moja Afrika, Aliko Dangote yupo katika mchakato wa kujenga kiwanda kikubwa cha kusafisha mafuta ghafi katika eneo la Afrika Mashariki.

Kiwanda hiki kinatarajiwa kuleta mapinduzi katika eneo la nishati kwani kitawezesha nchi za Afrika Mashariki kuipata nishati hiyo kwa uhakika na kwa bei nafuu.

Kiwanda hicho kinachotarajiwa kuwa na uwezo wa kusafisha mapipa 700,000 kwa siku, kimepangwa kujengwa huko Lamu nchini Kenya, kikiwa ni kiwanda kikubwa cha aina hiyo nje ya Nigeria.

TTCL yapanua mtandao wa intaneti

Na Mwandishi WETU

KAMPUNI ya Mawasiliano Tanzania (TTCL), imezindua awamu ya pili ya upanuzi wa mtandao wake wa intaneti ya majumbani.

Awamu hii upanuzi huo unalenga kuwafikia wateja wapya wa majumbani 400,000. Upanuzi wa mradi huo umezinduliwa na Waziri wa Mawasiliano, Angellah Kairuki (pichani).

Mpango huo uliopewa jina la kibiashara la Faiba Mlangoni Kwako, tayari umeunganisha wateja wa majumbani 280,000 katika awamu ya kwanza.

TTCL inazindua mpango huo wakati taarifa zinaonyesha kuwa idadi ya Watanzania wanaotumia huduma za intaneti nchini imefikia milioni 62.8.

Lakini katika idadi hiyo, wateja ambao wameunganishwa kwa waya wa faiba majumbani ni 178,904 tu.

Akizindua mpango huo, Kairuki aliiagiza TTCL kuharakisha kazi hiyo ili kuhakikisha kuwa lengo lililowekwa linafikiwa haraka.

Aidha, alisisitiza kuwa kusambaa kwa huduma hiyo ya majumbani kuendane na kupungua kwa gharama zake ili kuwawezesha Watanzania wengi kumudu kuitumia huduma hiyo.

Pia aliiasa TTCL kuhakikisha kuwa intaneti hiyo inakuwa na ubora na kasi kubwa sambamba na huduma bora kwa wateja ili kuhakikisha kuwa wateja wanapata thamani ya fedha wanaotumia kulipia huduma.

Alisema mafanikio ya huduma hiyo hayapaswi kupimwa tu kwa kuangalia ukubwa wa eneo ambalo huduma imefikishwa, bali kwa idadi ya watumiaji wa majumbani ambao wameunganishwa na wananufaika na huduma hiyo.

Waziri Kairuki alitaka TTCL kusambaza huduma hiyo pia kwenye maeneo ya biashara, viwandani, shuleni, vyuoni, vituo vya afya na ofisi za serikali.

Alisisitiza kuwa hilo litawezekana iwapo TTCL itarahisisha taratibu za usajili, kupunguza muda wa mteja kusubiri kuunganishwa, na kuimarisha ubora wa huduma bila kusahau kuwa-

hudumia wateja wenye matatizo kwa wakati.

Kairuki aliweka vigezo ambavyo alisema TTCL inapaswa kuvizingatia ili kujihakikishia kuwa inatoa huduma stahiki kwa wateja wake.

“Vipimo vya ufanisi viwe ni idadi ya wateja waliounganishwa, muda wa kuunganishwa na huduma, kasi ya intaneti, upatikanaji wa huduma muda wote na kutatua matatizo ya wateja kwa haraka. Kama mkifanya hivi wateja wataridhika kwa sababu wataona thamani ya fedha waliyotumia kujiunga wameipata,” alisema.

Alisema jinsi dunia inavyozama kwenye teknolojia sasa hivi, intaneti yenye kasi kubwa siyo anasa, bali ni huduma muhimu na lazima katika uzalishaji wa kisasa, utoaji elimu na maarifa na pia katika shughuli za kiuchumi kama vile biashara na kwa wafanyabiashara wadogo wadogo.

Akisisitiza umuhimu wa huduma hiyo, Kairuki alisema hata huduma nyingi za serikali hivi sasa zinatolewa kupitia mitandao hivyo kuimarika kwa huduma hiyo kutawasaidia wananchi wanaotafuta huduma za serikali kuzifikia kwa haraka na wepesi.

Utekelezaji wa mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050, ambayo inalenga kuhakikisha kuwa asilimia 70 ya wananchi wote nchini wanaunganishwa na wanaotumia huduma za intaneti.

Aidha, dira hiyo inalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya huduma zinazotolewa na serikali zitolewe kupitia mtandao ifikapo 2050.



■ Uchambuzi

Kujiuzulu Dkt Nchimbi mwisho au mwanzo wa mgogoro?



Na Peter NYANJE

KUJIUZULU kwa Dkt. Emmanuel Nchimbi kutoka nafasi ya Makamu wa Rais kumeongeza machungu mengine ya kufukuzwa kwake uanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Hatua hiyo imezua mshituko, mshangao, wasiwasi na hofu kwa watu wengi.

Ingawa wengi wana uhakika kuwa hatua hiyo inaweza isilete migongano itakayosababisha hitilafu kubwa, lakini wachambuzi wanasema ni dhahiri kuwa jambo hilo litasababisha mtikisiko ambao - usipodhibitiwa vyema, unaweza kuliyumbisha taifa.

Dkt. Nchimbi alitangaza Agosti 25 kwamba angejiuzulu nafasi ya Makamu wa Rais na kustaafu siasa pamoja na utumishi wa umma kuanzia Septemba 4.

Katika barua yake kwa Rais Samia Suluhu Hassan, alisema amefikia uamuzi huo baada ya kujiridhisha kwamba Rais alitaka makamu mwingine wa rais. Rais Samia alikubali kujiuzulu kwake.

Siku iliyofuata, CCM ilitangaza kumvua Dkt. Nchimbi uanachama wakimvika tuhuma za kukiuka maadili, kanuni na taratibu za chama.

Ingawa wengi tulitarajia jambo kama hili kutokea, lakini wengi hawakutarajia litatokea kwa namna lilivyotokea au kwa kasi namna hiyo.

Ndio maana mfuatano huo wa matukio umeibua maswali kuhusu mambo yaliyokuwa yakitokea nyuma ya pazia.

Ingawa hakuna ushahidi uliowekwa wazi hadharani unaohitibisha kwamba Dkt. Nchimbi alilazimishwa kujiuzulu, lakini kauli yake kuwa alikuwa amejithibitisha kuwa rais alihitaji mabadiliko inaleta taswira kuwa kujiuzulu kwake hakukutokana na utashi wake, bali alisukumwa. Vivyo hivyo, ingawa hakuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai yanayosambaa kuhusu alipo au kwamba amezuiwa kufanya shughuli zake, ukimya uliotawala tangu kujiuzulu kwake, na wasiwasi ulioibuliwa na baadhi ya watu ambao walishawahi kukutwa na kadhia kama hizo, kumezusha hofu nyingine kuhusi ana na usalama wa kiongozi huyo mstaafu.

Waziri mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, ambaye wakati fulani alisema kuwa aliwahi kupokea vitisho kuhusu usalama wake baada ya kutoa maoni kuhusiana na masuala mbalimbali ya kisiasa, ni mmoja wa watu walioonesha hofu kuhusu usalama wa Dkt. Nchimbi.

Wengi wanakumbuka madhila yaliyowakuta watu kama Aboud Jumbe, ambaye baada ya “kujiuzulu” nafasi ya makamu wa rais, aliishia kuwekwa katika kifungo cha ndani nyumbani kwake Kigamboni.

Inaendelea Uk. 21

Uchambuzi ■

Kujiuzulu Dkt Nchimbi

Inatoka Uk. 20

Wengine wamemkumbuka Horace Kolimba ambaye alifariki katika mazingira yenye utata baada ya kuitwa kuhojiwa na chama chake huko Dodoma baada ya kukikosoa hadharani akiwa Katibu Mkuu.

Ombwe laibuka

Hata hivyo, ukiacha hofu hiyo, kasi na mazingira ya kuondoka kwa Dkt. Nchimbi vimeacha ombwe la kisiasa ambalo limezalisha zaidi minong'ono na kutoa tafsiri mbalimbali.

Muhimu zaidi, tukio hili limefufua swali la muda mrefu katika siasa za Tanzania; je, ndani ya CCM au serikali kuna nafasi ya kutofautiana kimtazamo kwa mwanasiasa mwenye cheo cha juu bila kuonekana kuwa anapingana na mwelekeo wa chama au serikali?

Kuna orodha ndefu ya viongozi wa aina hiyo, lakini wa mwisho anayekumbukwa sana ni Humphrey Polepole.

Kivuli cha Aboud Jumbe

Kwa Watanzania wengi, tukio la Nchimbi limefufua kumbukumbu za Aboud Jumbe, makamu mwingine wa rais ambaye safari yake ya kisiasa ilifikia kikomo kwa namna ya kushangaza baada ya kutofautiana na uongozi wa wakati huo.

Jumbe alijiuzulu (baadhi wanaamini kuwa kwa kulazimishwa) Januari 1984 akiwa Rais wa Zanzibar, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu Mwenyekiti wa CCM, wakati kukiwa na mvutano mkubwa kuhusu mustakabali wa Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar.

Msimamo wake wa kuunga mkono muundo wa Muungano wa serikali tatu ulimweka katika mvutano na mfumo wa serikali mbili uliokuwa ukiungwa mkono na chama. Baada ya kujiuzulu, uhuru wake wa kisiasa na kijamii ulizuiwa kwa kiasi kikubwa, na hatimaye akaishi nje ya kitovu cha siasa hadi alipofariki mwaka 2016.

Kwa muda sasa kumekuwa na minong'ono kuwa kauli za Dkt. Nchimbi, hasa kuhusu Kati-

ba Mpya, ni moja ya mambo yaliyochochea kutoelewana kwake na baadhi ya vigogo wenzake ndani ya CCM na serikali.

Ndio maana kujiuzulu kwake kunaonekana kuwa ni kwa kulazimishwa na hakukutokana na utashi wake binafsi.

Ulinganisho huo unatiwa nguvu kwa sababu visa vyote viwili vinamhusu mwanasiasa mwenye cheo cha juu ndani ya mfumo wa utawala ambaye msimamo wake wa kisiasa ulionekana kukinzana na mwelekeo ndani ya chama na serikali.

Ndiyo maana kauli za Jaji Mkuu mstaafu Joseph Warioba zimevuta hisia. Warioba, ambaye pia ni mwanasiasa mkongwe wa CCM na Waziri Mkuu mstaafu, alihoji msingi wa madai kwamba Nchimbi anaweza kuwa kizuizini, huku akitambua kwamba kutokuwepo kwake hadharani kumezua wasiwasi.

Wasiwasi huo wenyewe ni jambo la kuzingatiwa. Katika mfumo wa kisiasa ambao bado una kumbukumbu za migogoro ya ndani ya chama, kutokuonekana hadharani kwa mwanasiasa maarufu kunaweza kugeuka kuwa suala la maslahi ya umma.

Katiba Mpya, mvutano wa kisiasa

Msimamo wa Dkt. Nchimbi kuhusu mabadiliko ya Katiba ni sehemu nyingine ambayo inaelezwa kuwa imechochea mazingira ya kuondoka kwake.

Inaendelea Uk. 22



■ Uchambuzi



Kujiuzulu Dkt Nchimbi

Inatoka Uk. 21

Mwezi Julai, Dkt. Nchimbi alisikika akiwataka Watanzania kupambana kudai Katiba Mpya. Aliuaminisha umma kuwa hilo ni takwa la Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa mtazamo mpana, msimamo huo ulikwenda sambamba na mjadala wa kisiasa nchini, kwa kuwa suala la Katiba Mpya limekuwa sehemu ya mijadala ya siasa Tanzania kwa miaka mingi na pia limewahi kutajwa hata katika ilani za CCM. Pengine ndio maana Dkt. Nchimbi akatoa kauli kuwa hata Rais naye anaitamani Katiba Mpya.

Lakini siku chache baadaye ikaanza kusikika minong'ono kuwa “wakubwa” kadhaa ndani ya CCM na serikali hawakufurahishwa na kauli hiyo.

Baadhi walihoji hadharani kuwa Dkt. Nchimbi anataka watanzania wapambane na nani!

Jambo moja ni dhahiri. Katika migongano ya kisiasa kuhusiana na suala la Katiba Mpya, kauli ya Dkt. Nchimbi, ambaye alikuwa Makamu wa Rais aliyekuwa madarakani, ilikuwa na uzi-to mkubwa zaidi kisiasa, pengine kuliko hata mashinikizo ya miaka mingi ya wanasiasa wa upinzani na wanaharakati.

Kwa hiyo, ingeshangaza kama isingezua mjadala, hasa katika kipindi ambacho mabadiliko ya Katiba ni miongoni mwa masuala nyeti yanayoikabili Tanzania.

Suala hilo pia linaingiliana na uhusiano kati ya CCM na taasisi zenye ushawishi nje ya chama.

Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), kwa mfano, limekuwa likitoa kauli kuhusu utawala, demokrasia, mabadiliko ya Katiba na masuala mengine ya kitaifa.

Mtazamo wa Dkt. Nchimbi kuhusu baadhi ya mijadala hiyo umeongeza tafsiri kuhusu uwepo wa tofauti za kisiasa ndani ya mfumo wa uongozi, huku baadhi ya wanasiasa wakimnasibisha Dkt. Nchimbi na TEC, hasa kwa kuwa naye ni Mkatoliki kindakindaki.

Athari kwa CCM

Ukizingatia kuwa haya yanatokea wakati ambapo CCM inajiandaa kwa uchaguzi ndani ya chama, kuondoka kwa Dkt. Nchimbi, ambaye amewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, ni dhahiri kutaleta misugvano.

Uzoefu unaonesha kuwa chaguzi hizi hutumiwa na baadhi ya watu wenye dhamira ya kuwania vyeo vya juu ndani ya chama au serikali kupanga safu kuelekea uchaguzi mkuu, wakitafuta uungwaji mkono.

Inaendelea Uk. 23

Uchambuzi ■

Kujiuzulu Dkt Nchimbi

Inatoka Uk. 22

Kwa miongo kadhaa, chama hicho kimeweza kusimamia makundi yenye maslahi tofauti, matarajio ya kisiasa na mitandao ya uongozi, huku kikidumisha utawala wake.

Wanasiasa wakuu wamepanda na kushuka, miungano ya kisiasa imebadilika na makundi yameibuka na kutoweka, lakini CCM imeendelea kuonyesha uwezo wa kujipanga upya.

Ndio maana kuvuliwa kwa Dkt. Nchimbi uanachama kunatafsiriwa na baadhi ya wachambuzi kama sehemu ya upangaji upya wa safu ndani ya chama kuelekea uchaguzi mkuu.

Baadhi ya wachambuzi wamehusisha kuondoka kwake na kupungua kwa ushawishi wa mitandao ya kisiasa ambayo wakati mmoja ilikuwa na nafasi muhimu katika michakato ya uchaguzi wa viongozi ndani ya CCM. Iwapo tafsiri hiyo ni sahihi, muda ndio utakaothibitisha.

Kitu kilicho wazi, hata hivyo, ni kwamba Tanzania inaingia katika kipindi ambacho maswali na majadiliano kuhusu nani anadhibiti chama, nani anaunda mwelekeo wa sera na nani anashikilia nafasi muhimu za kimkakati yatazidi kuwa muhimu.

Mchakato ujao wa kisiasa ndani ya chama, kwa hiyo, utafuatiliwa kwa karibu.

Swali jingine kubwa ni iwapo kuondoka kwa Dkt. Nchimbi ni mgogoro wa mtu mmoja au ni sehemu ya upangaji upya mpana zaidi wa mfumo wa kisiasa kuelekea chaguzi zijazo na mchakato wa urithi wa uongozi ndani ya chama na serikali.

Ni mtihani mkubwa zaidi

Suala la kujiuzulu kwa Dkt. Nchimbi linaenda mbali zaidi ya hatima yake binafsi.

Tukio hili limeipa CCM fursa ya kuonyesha namna chama kikubwa na chenye muda mrefu madarakani kinavyoweza kushughulikia tofauti za kimtazamo miongoni mwa viongozi wake wakuu.

Kila chama cha siasa kinahitaji nidhamu, lakini mfumo wa kisiasa uliokomaa pia unahitaji njia ambazo tofauti za maoni zinaweza kuwasilishwa bila moja kwa moja kutafsiriwa kuwa tishio kwa mustakabali wa mwanasiasa.

Kwa Tanzania, suala hili ni muhimu kwa sababu CCM si chama cha kawaida tu. Kikiwa madarakani tangu uhuru, mienendo yake ya ndani ina athari kubwa kwa serikali na jamii kwa ujumla.

Kwa hiyo, kuondoka kwa Dkt. Nchimbi hakutakuwa tu mabadiliko ya kawaida ya uongozi, bali kutaumba historia ndefu ya mamlaka, utii na kutofautiana ndani ya CCM.

Hapa, watu wasijikite tu kuhusu hatima ya Dkt. Nchimbi bali pia namna CCM itakavyoweza kuogelea katika wimbi hili.

Kwa upande mwingine serikali nayo ina mtihani wa itakavyoshughulikia maswali kuhusu hali ya Dkt. Nchimbi baada ya kuondoka madarakani, na iwapo viongozi waandamizi wataendelea kuwa na nafasi ya kueleza mitazamo inayotofautiana.

Historia imetoa mifano kadhaa ya namna tofauti za kimtazamo ndani ya uongozi wa juu zinavyoweza kugeuka kuwa migogoro mikubwa zinapogeuka kuwa masuala ya mtu binafsi.

Kuondoka kwa Nchimbi kumeifufua historia hiyo na

changamoto kwa uongozi wa sasa ni kuhakikisha kwamba historia isiendeleo kujirudia.



■ **Kilinge cha Mawasiliano**

Na Loth MAKUZA

Kwanini biashara ndogo zinahitaji PR?



WIKI iliyopita rafiki yangu, Juma, alinipa lifiti kwenye gari lake la zamani. Nyuma kulikuwa na vitanda viwili ambavyo alivitengeneza katika karakana yake ndogo maeneo ya Temeke.

Juma ni miongoni mwa mafundi seremala bora kabisa niliowahi kuwafahamu, kazi yake ni safi na mbao zake hazipasuki na bei yake pia ni nzuri.

Lakini anahangaika kulipa kodi, wakati duka kubwa la samani lililopo pembeni ya karakana yake, linalouza vitanda dhaifu vya kutoka nje, limefungua tawi la pili, maana biashara inakua.

Bidhaa dhaifu inashindaje? Tulipokuwa tunaendesha, nikamwambia ukweli. “Rafiki yangu, ngoma isiyopigwa ni kipande cha mti tu.” Akakaa kimya kwa muda.

Hilo ndilo funzo gumu ambalo biashara ndogo na za kati hujifunza kwa kuchelewa. Kuwa bora hakutoshi, watu lazima wajue kwamba wewe ni bora na nyenzo inayoeneza habari hiyo, kimyakimya na kwa gharama nafuu, ni mahusiano ya umma, yaani PR.

Ndio maana bidhaa bora si mara zote ndiyo inayoshinda; inayojulikana zaidi ndiyo hushinda.

Kuna maelfu ya kina Juma hapa nchini ambao ni mafundi nguo, wapishi, mafundi magari na wakulima wenye kazi zinazoweza kusimama sambamba na chochote kutoka nje.

Katika biashara, ukimya ni sawa na kutoonekana na duka lisiloonekana haliwezi kuuza bidhaa zake.

Hapa ndipo PR inashinda matangazo, unapolipia tangazo, kila mtu anajua unajisifu mwenyewe,

lakini gazeti, mtangazaji wa redio au ukurasa unaoaminika mtandaoni unapozungumza kuhusu biashara yako, kuna uzito.

Watu wanafikiri, “kama waliaamua kumwandika, basi lazima ni mzuri.” Uaminifu huo wa kuazi-ma huwezi kuununua kwa pesa moja kwa moja na ndio hasa biashara ndogo inahitaji ili kusimama sambamba na makampuni makubwa.

Fikiria kituo cha redio kikimtambulisha Juma kama “kijana anayetengeneza samani za kiwango cha kimataifa Temeke.” Hadithi hiyo moja ingefanya zaidi ya mwaka mzima wa kazi ya kimya.

Juma alijifunza ufundi kutoka kwa marehemu baba yake. Anawafundisha yatima wawili wa mtaa wake, anadhamini kila kitanda kwa miaka mitano. Hayo si maneno mazuri tu; ni sababu za kumchagua yeye badala ya muuzaji asiyejulikana.

Hadithi nzuri ya PR inambadilisha mgeni kuwa jirani. Watu hawanunui kitanda tu.

Wanamnunua mtu aliye nyuma yake. Ukisimulia hadithi hiyo vizuri, bei inaacha kuwa kitu pekee kinachohesabika.

Leo, mtu anapohitaji samani, hatembeji mitaani. Anafungua simu yake na kutafuta. Kama jina la Juma halionekani mtandaoni, basi kwa mteja huyo hayupo kabisa.

Lakini blogu, magazeti ya mtandaoni na kurasa za mitandao ya kijamii zinapotaja karakana yake, jina lake linaanza kuonekana kwenye Google.

Hii ndiyo sehemu ninayoipenda zaidi. Juma hatawahi kutumia pesa kuliko duka kubwa lakini anaweza kuwazidi akili.

Tangazo linakufa mara pesa zinapoisha. Hadithi ya kweli inaendelea kutembea kwa miguu yake yenyewe.

Kwa muda sasa kwenye tasnia hii ya mawasiliano, nimeliona hili mara nyingi mno. Biashara zinazokua si mara zote ndizo zenye ujuzi zaidi ni zile zenye ujasiri wa kusikika.

Adui yako halisi siyo kampuni kubwa yenye duka linalong’aa, bali ni ukimya wako.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@lothmakuza.co.tz

Na Emmanuel JACOB



Afya ya Kimwili ■

Fiziotherapia huimarisha maisha, uhuru

KATIKA jamii nyingi hasa Afrika, ulemavu huonekana kama kikwazo kinachomzuia mtu kuishi maisha yenye tija na furaha.

Ukweli ni kwamba, ulemavu sio mwisho wa maisha au kikomo cha ndoto za mtu.

Huduma za fiziotherapia (wengi huita mama cheza) zina mchango mkubwa na wa kipekee katika kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata fursa ya kufurahia ubora wa maisha, kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Kwa mtu anayeishi na ulemavu iwe wa kuza-liwa, uliotokana na ajali au ugonjwa kama vile kiharusi (stroke), wataalamu hutumia mbinu za kisayansi, mazoezi maalum na vifaa saidizi ili kusaidia mwili kurejesha uwezo wake.

Kwa wasomaji wa gazeti la Pambazuko makala haya yanaangazia baadhi ya faida katika mae-neo.

Kwanza, kurahisisha uwezo wa kutembea na kupunguza maumivu. Mazoezi ya viungo husaidia kuongeza nguvu za misuli, kuboresha uratibu wa mfumo wa fahamu na viungo, pamoja na kupunguza maumivu ya muda mrefu yanayoweza kumpata mtu mwenye ulemavu.

Pili, kujenga uhuru na kujitegemea, kupitia tiba hii, mtu hufundishwa mbinu mpya za kufanya mambo ya kila siku kama vile kujivalisha, kula, au kutoka sehemu moja kwenda nyingine bila kulazimika kutegemea msaada wa wengine muda wote.

Tatu, kuzuia madhara mengine ya kiafya: Mtu anayetumia kiti cha magurudumu au aliye kitandani kwa muda mrefu yuko katika hatari ya kupata vidonda vya kukaa (bedsores), kupinda kwa mifupa (contractures), na matatizo ya mzunguko wa damu.

Fiziotherapia huzuia changamoto hizi kabla hazijatokea.

Nne, kukuza afya ya akili na kujiamini. Uwezo wa kujisogeza na kufanya mambo binafsi huongeza kujiamini, kupunguza msongo wa mawazo au mshtuko wa nafsi na kuwapa watu wenye ulemavu matumaini ya siku zijaye.



Huduma imara hupunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa muda mrefu kwa kuwasaidia watu wenye ulemavu kukuza uwezo wao wa kimwili, kujiamini, na kujitegemea.

Hii ina maana kwamba, ingawa watu wenye ulemavu wataendelea kuwepo katika jamii zetu, hawapaswi kuonekana kama ombaomba au mzigo, bali kama wajumbe wenye uwezo wa kujitegemea.

Fiziotherapia sasa inaleta mabadiliko makubwa ya mtazamo kutoka kwenye dhana ya kutegemea matibabu ya hospitalini pekee, hadi kumwezesha mtu binafsi kupata uhuru na uwezo wa kumudu maisha yake ya kila siku.

Kama inavyosisitizwa katika kaulimbiu za kimataifa za afya, kila mtu ana haki ya kuishi maisha hai na yenye ubora.

Fiziotherapia si tu huduma ya matibabu bali ni daraja linalowavusha watu wenye ulemavu kutoka kwenye utegemezi na kuwafikisha kwenye uhuru na utu wao.

Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob.

■ **Bustani ya Sheria****Na Wakili Karim Gabriel Mussa**

Sakata la Wakili Fatma Karume – VII

SEHEMU ya sita tuliona jinsi serikali ilivyoendelea kupambana Mahakama ya Rufani kwa kuomba ruhusa ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu uliotengua uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Mawakili.

Lakini wakati huohuo, Fatma Karume naye alikuwa ameanzisha vita vyake tofauti kabisa mbele ya Mahakama ya Rufani.

Safari hii hakulalamikia Kamati ya Maadili, alikuwa analalamikia uamuzi wa kwanza kabisa wa Jaji Eliezer Feleshi uliomsimamisha kwa muda kufanya kazi ya uwakili wakati akiwa anamwakilisha Ado Shaibu.

Fatma Alienda Mahakama ya Rufani kwa njia gani? Kwani yeye hakukata rufaa, badala yake, alifungua maombi ya revision (mapitio), akiiomba Mahakama ya Rufani iingilie kati na kutengua uamuzi wa Mahakama Kuu uliomsimamisha kwa muda kufanya kazi ya uwakili. Hoja yake ilikuwa kwamba uamuzi huo haukuwa sahihi kisheria na ulipaswa kufutwa, lakini kabla Mahakama ya Tanzania haijachunguza kama alikuwa sahihi au la iliibuka swali moja la msingi.

Je, revision ndiyo ilikuwa njia sahihi ya kufika Mahakama ya Rufani?

Mahakama ya Rufani nayo ilijibu baada ya kuchambua Sheria ya Mawakili, Mahakama ya Rufani ilisema hapana. Mahakama ikaeleza kwamba kifungu cha 22(2)(b) cha Sheria ya Mawakili tayari kilikuwa kimeweka utaratibu maalumu wa kupinga uamuzi wa Jaji aliyemsimamisha wakili kwa muda.

Kwa hiyo, kabla ya kwenda Mahakama ya Rufani, Fatma alipaswa kwanza kutumia utaratibu huo wa kisheria. Kwa maneno mengine alikuwa amekimbil-ia Mahakama ya Rufani kabla ya kutumia njia ambayo sheria ilikuwa imeitenga mahsusi kwa aina hiyo ya malalamiko.

Kwa sababu hiyo, Mahakama ya Rufani haikuingia kujadili kama Jaji Feleshi alikuwa sahihi au alikosea.

Badala yake, ilisema njia iliyotumika haikuwa sahihi Na hivyo maombi ya revision yakashindwa.

Je, hatima ya Fatma Karume ikawa nini? Na hili ndilo swali ambalo wengi huuliza, baada ya kupitia kesi zote saba. Ni kweli kwamba Mahakama Kuu ilitengua uamuzi wa Kamati ya Maadili uliokuwa umemfuta Fatma Karume kabisa kwenye Daftari la Mawakili. Lakini, Mahakama haikumrudishia moja kwa moja leseni yake ya uwakili, kwa sababu Mahakama ilisema

kilichoharibika ni utaratibu wa kufikisha shauri mbele ya Kamati, si lazima iwe kwamba madai yenyewe hayakuwa na msingi.

Ndiyo maana ikaagiza Msajili wa Mahakama Kuu ndiye afikishe suala hilo kwenye Kamati ya Maadili kwa kufuata utaratibu uliokuwa umeelekezwa tangu mwanzo. Kwa mujibu wa taarifa zilizopo hadi sasa, uamuzi huo bado haujazaa hitimisho jipya linalomaliza kabisa suala hilo. Hivyo, hali iliyobaki kusimama ni ile ya uamuzi wa awali uliomsimamisha Fatma Karume kwa muda kufanya kazi ya uwakili, kwa kuwa uamuzi wa Kamati uliomfuta kabisa ulifutwa, lakini suala lenyewe halikufungwa kwa uamuzi mpya wa mwisho.

Mafunzo muhimu katika sakata hili

Mfululizo wa mashauri haya saba yamekuwa miongoni mwa mashauri muhimu zaidi katika sheria za maadili ya uwakili nchini Tanzania.

Zimefundisha mambo kadhaa muhimu ambayo ni pamoja na utaratibu wa kisheria ni muhimu kama haki yenyewe. Hata kama madai yana uzito, yakiletwa kwa utaratibu usio sahihi yanaweza kubatilishwa.

Wakili ana uhuru wa kumtetea mteja wake kwa nguvu zote za sheria, lakini uhuru huo unaambatana na wajibu wa kuheshimu maadili ya taaluma na taasisi za haki. Mahakama haiangalii tu nani ana hoja nzuri, bali pia kama sheria na taratibu zimefuatwa.

Kuchagua nafuu sahihi ni jambo la msingi. Ukichagua njia isiyotambuliwa na sheria, unaweza kupoteza shauri bila Mahakama hata kuingia kwenye kiini cha malalamiko yako.

Hitimisho

Sakata la Wakili Fatma Karume si simulizi ya mtu mmoja pekee, ni simulizi kuhusu mgongano kati ya uhuru wa wakili kutetea mteja wake kwa nguvu zote, mamlaka ya mahakama kusimamia maadili ya taaluma, na umuhimu wa kufuata taratibu za kisheria.

Ndiyo maana hadi leo, kesi hizi zinaendelea kufundishwa katika Law School of Tanzania, vyuo vikuu na mijadala ya kitaaluma, kwa sababu zinagusa misingi mikuu ya Legal Ethics, Civil Procedure na Constitutional Litigation.

Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com

Na Rashid MTAGALUKA



Hoja Yangu ■

Wapangaji wanapobadilishana, nyumba haipaswi kubomoka

MABADILIKO ya viongozi katika nchi yoyote ni jambo la kawaida. Leo mtu anaweza kuwa madarakani, kesho asiwepo. Leo anaweza ku-shika nafasi kubwa, kesho nafasi hiyo ikawa mikononi mwa mwingine. Huo ndio uzuri na wakati mwingine ugumu wa uongozi wa kisiasa.

Lakini swali muhimu si nani ameondoka au nani ameingia. Swali ni je, taasisi inabaki imara baada ya mtu (kiongozi) kuondoka?

Tukio la kujiuzulu kwa aliyekuwa Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, na badaye kupatikana kwa Deogratius Ndejemi ku-shika nafasi hiyo, limetukumbusha jambo moja kubwa kuhusu uongozi wetu.

Jambo lenyewe ni kwamba, kumbe nchi haiwezi kujengwa kwa kutegemea mtu mmoja. Na kiongozi mzuri si yule anayefanya taasisi ionekane imara kwa sababu yupo, bali yule anayesaidia kujenga mfumo ambao utaendelea kuwa imara hata yeye akiwa hayupo.

Hapa ndipo tunapaswa kujiuliza kama Tanzania tunajenga taasisi zinazowatumikia viongozi, au viongozi wanaotumikia taasisi? Na ndipo Hoja Yangu wiki hii ilipojikita. Kwamba, tunahitaji viongozi wanaoondoka na kuiacha taasisi na uimara wake.

Mabadiliko ya uongozi yasitafsiriwe kila mara kama tetemeko la kisiasa. Kama mifumo yetu ni imara, kuondoka kwa kiongozi mmoja hakupaswi kusababisha hofu kwamba mambo yote yatabadilika. Hapana!

Viongozi wanakuja na kuondoka, lakini Katiba, serikali, bunge, mahakama na taasisi nyingine za umma vinapaswa kubaki.

Jambo lingine muhimu ni kuhakikisha kuwa mabadiliko ya viongozi hayaathiri mwendeleo wa sera na mipango ya maendeleo. Wananchi hawapaswi kuanza upya kila mara kiongozi anapobadilika. Serikali si mradi wa mtu binafsi; ni chombo kinachoendelea kuhudumia wananchi, licha ya mabadiliko ya wanaokiongoza.

Aidha, viongozi wanapaswa kujenga mazingira ya kuwaachia madaraka kwa heshima.

Kuondoka si kushindwa, na kuingia madarakani si ushindi wa mtu binafsi. Vyote ni sehemu ya mzunguko wa uongozi unaopaswa kuheshimu taasisi na maslahi mapana ya taifa.

Ni muhimu pia kujenga utamaduni ambao kiongozi anaweza kuondoka madarakani bila kuonekana kama ameangusha nchi. Na zaidi, anayechukua nafasi yake asionekane kama ameingia kwenye ofisi iliyokuwa mali ya mtangulizi wake. Ofisi ni ya wananchi, si ya mtu.

Hili ni somo muhimu kwa wanasiasa wetu. Mamlaka ni dhamana, si urithi. Nafasi ni ya muda, lakini taasisi ni ya kudumu.

Tanzania inahitaji viongozi wanaojua kwamba historia haitawakumbuka kwa muda walio-kaa madarakani pekee, bali pia kwa aina ya taasisi walizoacha nyuma yao.

Kwa hiyo, tusitumie mabadiliko ya viongozi kujenga hofu. Tuitumie kama nafasi ya kupima uimara wa mifumo yetu na uwezo wa taifa kuendelea mbele bila kutegemea umaarufu au nguvu ya mtu mmoja.

Kwa sababu mwisho wa yote, viongozi ni wasafiri, taasisi ni nyumba. Wasafiri wanapobadilishana, nyumba haipaswi kubomoka.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



■ Mazingira

Ujenzi wa ukuta wa kilomita mbili Msitu wa Ngezi wakera



Na Mwandishi WETU

UKUTA kuzunguka mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano ndani ya Msitu wa Ngezi, Pemba unakera wananchi.

Katika mradi huo wenye uwekezaji wa Shilingi bilioni 17.4 wa hoteli ya kitalii inayomilikiwa na Kampuni ya WIPI Group kutoka China, unalalamikiwa na wananchi kwamba unazinga ustawi wao, ikiwamo kuwanyima njia walizozoea kupita kwa miaka mingi.

Ukuta huo wa kilomita mbili, unajengwa kuzunguka mradi wa hoteli hiyo.

Wakazi wa Jimbo la Konde, maofisa wa idara ya misitu, watafiti na wanaharakati wa mazingira kisiwani Pemba wameiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Mamlaka ya Kuendeleza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kusitisha ujenzi huo kwani unaharibu mazingira na kutishia shughuli za utalii na kiuchumi miongoni mwa wananchi.

Katika taarifa yake wiki iliyopita, kiongozi wa watafiti wa mazingira kutoka Chuo Kikuu

cha Bristol nchini Uingereza, Profesa Tim Caro amesema ujenzi wa ukuta huo ambao ni uzio katika eneo ambalo Hoteli ya Mantuli Eco-Resort inajengwa, pia unazuia shughuli za doria za maofisa misitu katika msitu huo na shamba la mpira la Vumawimbi.

“Ukuta huo pia ni pingamizi katika shughuli za kiuchumi za wananchi kama vile uvuvi, kuongoza watalii katika hifadhi, lakini pia unazuia wananchi kufika katika fukwe za Bahari ya Hindi kwa ajili ya mapumziko,” Prof Caro amesema katika taarifa yake.

Ujenzi wa ukuta huo kwa kutumia matofali yaliyofyatuliwa kijiji cha jirani cha Makangale ulianza mwishoni mwa mwaka jana na kuzua taharuki miongoni mwa wananchi na wanaharakati wa mazingira.

“Malori na mitambo ya ujenzi vimeondoka, lakini bado kuna kibao kirefu chenye maandishi ya Mantuli Eco-Resort na ramani ikionyesha mipaka ya eneo la mradi ambalo asilimia 23 ni eneo la Msitu wa Hifadhi wa Ngezi,” ilisema taarifa hiyo ya Prof Caro.

Taarifa hiyo ilifafanua kwamba pamoja na maelezo ya maofisa wa ZIPA kwamba ujenzi huo utafanyika zaidi kwenye shamba la mpira la Vumawimbi, hakuna ramani wala maandishi yoyote yanayothibitisha jambo hilo zaidi ya maelezo ya mwekezaji.

Katika taarifa hiyo, Prof

Caro ameonya kwamba ujenzi huo utaathiri mazingira ya viumbehai wakiwemo wadudu, mimea, wanyama na ndege ambao hawapati kani sehemu yoyote duniani jambo ambalo lita-punguza utalii wa mazingira.

“Kwanza, hifadhi ya msitu huu ina aina nane za mimea ambayo ni ya kipekee katika sayansi ya utafiti na mpaka sasa haipatikani popote Afrika isipokuwa Ngezi,” ilisema ripoti hiyo.

Inaendelea Uk. 29

Mazingira ■

Ujenzi wa ukuta...

Inatoka Uk. 28

Pamoja na mimea hiyo ya pekee, Msitu wa Hifadhi wa Ngezi una miti mirefu yenye umri wa miaka zaidi ya 100 pamoja na mnyama mdogo aina ya mbalawa wa blu ambaye hayupo popote hapa Afrika.

Wakati shughuli za kusafisha eneo la ujenzi zinaanza mwezi Septemba mwaka jana, wanaharakati wa mazingira, watafiti na wananchi walipinga mradi huo wakisema utaathiri shughuli zao za maendeleo.

“Ujenzi huu ndani ya Hifadhi ya Msitu wa Ngezi unatishia kuharibu mazingira na kuathiri viumbehai ambayo ndiyo kivutio kikuu cha watalii na chanzo cha mapato ya wananchi wengi hapa Konde,” alisema Abdurahman Mbaruk, katibu wa taasisi ya wanaharakati ya Ngezi Natural Resources Conservation Organization.

Mbaruk anasema ujenzi wa hoteli hiyo tayari unaathiri shughuli za uhifadhi na utalii katika msitu huo ambao watafiti wanasema una upekee katika Afrika.

Ameomba uongozi wa ZIPA kuwashirikisha wakazi wa eneo hilo katika uwekezaji huo ili kupata maoni yao namna ya kuboresha mradi huo kwa manufaa ya jamii ya eneo hilo ambayo baadhi yao ni waongoza watalii.

Mjumbe wa bodi ya Tanzania Forest Conservation Group, Thabit Masoud aliunga mkono hoja hiyo akisema mradi huo wa hoteli ya kitalii utazorotesha shughuli za uhifadhi na kuathiri maisha ya watu wa Konde ambao wengi wao ni wakulima na wavuvi.

“Tangu miaka ya tisini ujenzi wa hoteli za kitalii ndani ya msitu umepamba moto na manufaa yake kwa wananchi bado kuonekana, ni vyema sasa kuwepo kwa mazungumzo ambayo yataleta amani na maendeleo kwa wahusika wote,” alisema Masoud huku akishauri ZIPA kuhamishia mradi huo kwende eneo jingine.

“Mradi kama huu unahitaji kushirikisha wananchi ili kuleta manufaa kwani wawekezaji wakishajenga hoteli hawashirikiani na wananchi kama wanavoahidi kabla,” alisisitiza huku

akishauri kwamba ni vyema serikali ikahamisha mradi huo ambao umekuwa kimya siku za karibuni baada ya wanaharakati kushinikiza uondoke eneo hilo.

Idara ya Misitu Kisiwani Pemba ilisema katika ripoti yake mwishoni mwa mwaka jana kwamba ujenzi wa ukuta huo umezuia shughuli za doria kwani umeziba njia za kupita askari wa idara hiyo na pia maafisa utalii.

Katika ripoti yake ya Desemba 18, 2025 ambayo ilipelekwa kwa Mkurugenzi wa Misitu - Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na nakala kwa Katibu Mtendaji wa ZIPA, idara hiyo ilisema kwamba mradi huo ulikiuka baadhi ya taratibu za uwekezaji za wizara.

“Hatupingi mradi huu kwani serikali inayo nia njema ya kukuza utalii ila ni vyema taratibu za wizara za uwekezaji katika eneo la hifadhi zifuatwe,” ilisema ripoti hiyo ambayo Katibu Mtendaji wa ZIPA, Saleh Saad Mohamed aliwaahi kuikana.

“Mie sijaona ripoti hiyo ila naweza kusema kwamba hakuna tofauti kati yetu na Idara ya Misitu kuhusu mradi huo ambao ni mpango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendeleza utalii kisiwani Pemba,” alisema Mohamed.

Alisisitiza kwamba mradi huo una manufaa makubwa kwa uchumi wa Pemba na Zanzibar kwa ujumla kwani unaboresha miundombinu ya utalii ili kuongeza idadi ya watalii wanatembelea kisiwa hicho cha pili kwa ukubwa visiwani Zanzibar.

Hoja yake iliungwa mkono na mwakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zawadi Amour Nassor ambaye alisema wakati Unguja inapokea watalii zaidi ya laki tano, Pemba inapata wasiozidi laki moja kwa mwaka.

“Moja ya tatizo kubwa ni ukosefu wa hoteli za kitalii kwa hiyo mradi huu unalenga kutatua changamoto hiyo,” alisema Nassor ambaye alipinga madai ya wananchi wa jimbo lake kwamba hawakushirikishwa katika kupitishia mradi huo.

“Wanaotoa madai hayo ni wale ambao hawaji kwenye mikutano tukiitisha kwani jambo hili tulijadili kwenye mikutano ya hadhara,” alisema mwakilishi huyo huku akiwataka wakazi hao kuunga mkono jitihada hizo za serikali.

■ Barua za Wasomaji



Tunakaribisha barua. Tuma kupitia

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba;
+255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

Kelele za baa zinatukosesha usingizi

Mhariri,

KWA niaba ya wakazi wa eneo la Mbagala Kizuiani jijini Dar es Salaam, natoa dukuduku kuhusu uwepo wa kelele za muziki kwenye baa zinazotuzunguka.

Mhariri sisi wananchi wa Mbagala-Kizuiani, tunakerwa na kelele za muziki unaopigwa kwa sauti ya juu kuanzia jioni hadi usiku mwingi jambo linaloleta kero kwa watu tunaoshi maeneo ya jirani.

Watoto wetu wanashindwa kusoma kwa utulivu lakini pia wagonjwa na wazee wanateseka kutokana na kelele hizo.

Mara kadhaa tumejaribu kuzungumza na wamiliki wa baa hizo, lakini hakuna mabadiliko yoyote hadi sasa.

Tunaelewa biashara ni muhimu, lakini pia tuna haki ya mazingira tulivu nyumbani.

Sheria ya Mazingira inatoa viwango vya kelele vinavyopaswa kufuatwa.

Tunaomba mamlaka husika kutoa elimu kwa wamiliki wa baa wafanye ukaguzi wa mara kwa mara ili kudhibiti hali hiyo.

**Ahmed Jumaa,
Mkazi wa Mbagala,
Dar es Salaam.**

Daladala zinazokatisha ruti zidhibitiwe

Mhariri,

NAOMBA kuleta malalamiko kuhusu tabia ya baadhi ya usafiri wa daladala kukatisha ruti njiani jambo ambalo linawatesa abiria.

Kila siku asubuhi na jioni abiria wengi husubiri daladala kwa muda mrefu vituoni jambo ambalo limekuwa tatizo kubwa.

Daladala nyingi zinapofika katikati ya safari yanakatisha ruti na kuwashusha abiria hovyoy. Mfano daladala ya Ubungo – Kariakoo, inaishia Magomeni na kutuambia tubadili magari.

Hii inatufanya tupoteze muda na pesa na kusababisha tulazimike kulipa nauli mara mbili lakini pia wengine hufika kazini na shuleni kwa kuchechelewa.

Naomba Latra na vyama vya madereva na wamiliki wa daladala vifuatilie suala hili ikiwezekana iwepo adhabu kali kwa dereva yeyote atakayekatisha ruti bila sababu. Abiria tunastahili huduma bora na ya uhakika.

**Mkereketwa,
Neema Jonas,
Dar es Salaam.**

TanESCO mnaupiga mwingi

Mhariri,

NAOMBA nitumie gazeti lako la Pambazuko kulipongeza Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (TanESCO) kwa huduma yao bora.

Nikiwa ni shuhuda wa hilo, mara kadhaa ninapokuwa na tatizo la umeme na pale ninapowapigia simu, wamekuwa wakitoa ushirikiano.

Mimi ni mkazi wa Kerege-Bagamoyo, niliomba huduma ya kufungiwa umeme Mei mwa-

ka huu, lakini kwa wakati ule waliniambia kuwa kuna changamoto ya nguzo hivyo ingechelewa.

Binafsi niliwelewa na tayari mwezi uliopita nguzo zilipopatikana wakanijulisha kwa meseji kuwa nitahudumiwa ndani ya siku kumi.

Ninawashukuru na kuwapongeza TanESCO kwa sababu tayari wametimiza ahadi yao waliyoitoa.

Kongole TanESCO, hakika mnaupiga mwingi.

**Mnufaika wa huduma,
Kerege, Bagamoyo**

Chem Chem yaibuka hoteli bora Afrika



Jorg Weytjens



Jennifer Giray

Mussa JUMA, Babati

HOTELI ya kitalii ya Chem Chem, imeshinda tuzo ya ubora Afrika – kwa mara ya pili mfululizo, katika tuzo zinazoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Utalii (WTA).

Chem Chem Safari Lodge iliyopo eneo la hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori (WMA) la Burunge, Wilaya ya Babati, Manyara ambalo lipo chini ya Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) imeshinda tuzo hiyo mfululizo mwaka 2025 na mwaka 2026.

Ushindi huu ni sehemu ya malengo ya muda mrefu ya waanzilishi wa hotel hiyo; Nicholas Negri na Fabia Bausch baada ya kuifanya Burunge WMA kuwa hifadhi ya jamii bora zaidi Afrika, kwa kutoa huduma bora za utalii, kuongezeka wanyamapori na kuwa na mazingira bora zaidi ya kufanya utalii wa kifahari.

Wakizungumza baada ya kukabidhiwa tuzo hizo mbili, wafanyakazi wa Chem Chem na viongozi wa

serikali Mkoa Manyara walisema mafanikio hayo ni mkakati wao wa muda mrefu.

Meneja Mkuu wa Chem Chem Safari, Jorg Weytjens amesema ushindi huo unathibitisha huduma bora wanazotoa na kuvutia watalii.

“Tunashukuru sana watalii kutoka sehemu mbalimbali duniani kuendelea kutupigia kura na kutupa ushindi kutokana na huduma bora tunazotoa,” anasema.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Babati Vijijini, Anna Mbogo anasema ushindi wa Chem Chem unadhihirisha ushirikiano baina ya serikali, wananchi wa vijiji 10 vinavyounda hifadhi hiyo na wafanyakazi wa Chem Chem.

“Sisi serikali tunapongeza ushindi huu kwani utaendelea kutangaza wilaya yetu ya Babati, lakini pia kuongeza mapato na kutimiza dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuvutia watalii Tanzania,” amesema.

Meneja Rasilimali watu wa Chem Chem, Jennifer Giray amesema ushindi waliopata unatokana na kuendelea kutoa huduma bora ambazo zinavutia watalii.

“Tunashukuru sana wakurugenzi wetu, Nicolas na Fabia kwa usimamizi mzuri, malengo makubwa waliotuwekea na sasa tunafanya vizuri Afrika,” amesema.

Amesema wafanyakazi wa hotel hiyo wanashirikiana kwa kiasi kikubwa na katika mazingira mazuri ambayo yanawavutia kutoa huduma bora.

Muongoza watalii wa Chem Chem, Isack Joseph amesema wanajivunia tuzo hiyo na kuahidi kuendelea kutoa huduma bora zaidi Kwa watalii.

Joseph amesema wataendelea kutoa huduma bora na kuvutia mamilioni ya watalii na hivyo kuongeza mapato ya hotel na kwa serikali.

Meneja wa huduma katika hotel hiyo, George Andrew amesema lengo lao wakati wote ni kutoa huduma bora Kwa watalii.

Hata hivyo, alipongeza ushirikiano ambao wanapewa na serikali kuanzia ngazi ya taifa hadi vijijini na hivyo kuwafanya watalii kuwa salama na wenye furaha wanapowatembelea muda wote.

Ushindi wa Chem Chem ulitangazwa katika hafla ya kutoa tuzo hizo zilizofanyika wiki iliopita Zanzibar.

■ Vituko vya Wakubwa

‘Maajabu’ ya Rais Mobutu akiwa Ikulu - II



Mobutu Sese Seko

Na Mwandishi WETU

MWAKA 1965 kulitokea mkasa mmoja huko Kinshasa, ambapo mwanamuziki maarufu nchini humo, Tabu Ley Rochereau (sasa marehemu) alipotunga wimbo ulioitwa “Kashama Nkoyi.”

Ndani ya wimbo huo, Tabu Ley aliweka maneno kama vile ‘boni oweleli, okende liboso ya baninga, soki okutani na Lumumba okoloba nini papa? tokengelaki yoo’ te Kashama Nkoyi.”

Kwa tafsiri isiyo rasmi ya kiswahili anasema; “inakuaje kusafiri, watutangulia sisi wenzio, huko uendako, utakapokutana na Lumumba utamwambiaje baba? wala hatujawahi kufanya uchunguzi wa kina kwa yale yaliyokukuta....” Kashama Nkoyi.

Wimbo huo baada ya kutoka ulipigwa marufuku na serikali ya Mobutu, siyo kwa sababu alitajwa Lumumba, bali kumetajwa jina la “Kashama Nkoyi.”

Serikali ya Mobutu ilimshutumu Tabu Ley kutumia jina hilo bandia kwa kumuenzi Pierre Mulele, ambaye alikuwa ndiye mtu pekee aliyekuwa anamsumbua kichwa rais huyo.

Mulele alikuwa mmoja kati ya mawaziri wa Emery Patrice Lumumba, shujaa wa uhuru wa Kongo baada ya kuuawa Lumumba.

Mulele alisimama kidete kupambana na Serikali ya Mobutu huku vikosi vya waasi vilivyokuwa vikitawala mashariki mwa Kongo hususan mikoa ya Kivu, vilikuwa vikimchukulia Mulele kama kiongozi wao mkuu.

Kutokana na harakati za Mulele, akaibuka Laurent Desire Kabila kuendeleza harakati zake zenye falsafa ya Lumumba.

Mulele aliuawa mwaka 1968 kwa kukatwa katwa vipande na askari wa Mobutu kwenye kambi ya “Tshatshi” ambayo ilikuwa na mako-mandoo maalumu wa kiongozi huyo.

Almanusra Tabu Ley naye auawe, lakini akaomba msamaha na kuahidi kuimba nyimbo za ‘mapambio’ kwa Mobutu. Mobutu akamsamehe na kumpa masharti ya kuwa kibaraka wake kupitia muziki.

Tabu Ley alizaliwa mwaka 1940 huko Bandundu katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Alikuwa mmojawapo wa wanamuziki wali-oimba ule wimbo wa ‘Grande Kalle’ uliotikisa anga la Afrika miaka ya 1960 na baadaye wimbo huo uliitwa “Independence Cha Cha”, ambao uligeuka kuwa wimbo rasmi wa kusherehekea uhuru wa Zaire.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990 Tabu Ley aliachia nyimbo kama muzina, exil Ley na babeti soukous na kuendelea kuheshimika ndani nan je ya Kongo kupitia muziki wake.

Vituko vya Wakubwa ■

‘Maajabu’ ya Rais...

Inatoka Uk. 32

Na baada ya utawala wa Mobutu kuanguka, Tabu Ley alipewa uwaziri katika utawala wa Laurent Kabila na hata baada ya kifo cha kiongozi huyo, Novemba, 2005 aliteuliwa na Joseph Desiree Kabila kwa kupewa cheo cha naibu gavana anayehusika na masuala ya kisiasa, utawala, jamii na utamaduni katika Jimbo la Kinshasa.

Aidha, mwaka 1967, Franco Luambo na wimbo wake “Luvumbu Ndoki,” kwenye lugha yake ya Lingala, ujumbe huo ulisema; “Wewe Luvumbu, mtu ambaye kijiji kizima kinakutegemea, wanakijiji wote wako chini ya usimamizi wako, umewamaliza ndugu zako wote, wa kike kama vile Fariki, nani yule atakayekuzika?”

Wimbo ukaendelea; “Mimi François nashindwa kabisa kulia, kwa kweli huwa najiuliza, kwani uchawi wako upo mgongoni au tumboni mwako?”

Wimbo huo pia ulipigwa marufuku mara moja pale ulipotoka hewani, Serikali ya Rais Mobutu ikasema kwamba kupitia wimbo huo, Franco kawatukuza wanasiasa wanne waliouawa kwa kunyongwa kwa madai kwamba walikuwa na nia ya kuipindua serikali mwaka 1966.

Baada ya wimbo huo kufungiwa, zikawepo tetesi kuwa Franco anatafutwa na serikali. Kusikia hivyo, Franco akakimbia pamoja na kundi lake wakajifadhi kwa muda jijini Brazzaville.

Akiwa huko, Rais Mobutu akamtumia ujumbe na kumshawishi arudi nyumbani Kinshasa na kumuahidi kuwa maisha yake hayatakua hatarini.

Franco alipopokea wito huo aliamua kurudi Kinshasa, lakini aliporudi tu alikaribishwa na kikosi cha wanajeshi maalumu wa Mobutu ambao waliwamuru yeye na kundi lake walipeleka kwa moja kwa moja jela ya Ndolo.

Huko walikaa kwa muda wa siku mbili, inasemekana walicharazwa bakora sawasawa na baadaye walitolewa jela ya Ndolo na kuhamishi-



wa kambi ya jeshi “Tshatshi” ambapo walishiki-liwa kwa siku kadhaa.


Rais Mobutu baadaye alikwenda mwenyewe kujadiliana na Franco na kumweleza kuwa kuanzia siku hiyo hadi siku atakapoondoka madarakani atakuwa akimwimbia yeye na kufanya kazi zake zote muda wote atakaomwitaji. Kuanzia siku hiyo, Franco akawa kiungo kikuu kwenye kampeni zote za Rais Mobutu.

Kutokana na ushirikiano huo, Franco alinufaika sana kuwazidi wanamuziki wengine wote wa nchi hiyo katika utawala wa Serikali ya Mobutu. Alifariki dunia nchini Ubelgiji Oktoba 12, 1989.

Hata hivyo, nyimbo za mwanamuziki huyo nguli zimeendelea kupendwa sana ndani na nje ya DRC, huku nyingine zikichukuliwa kama nembo ya taifa hilo.

Orodha ya wanasiasa waliopata kunyongwa na serikali ya Mobutu kwa nyakati tofauti ni pamoja na Jérôme Anany (waziri wa zamani wa ulinzi wa taifa, Emmanuel Bamba (Seneta), Evariste Kimba (waziri mkuu wa zamani) na Alexandre Mahamba (waziri wa ardhi).

Makala hii ambayio itaendelea wiki ijayo imeqandaliwa kwa msaada wa mitandao.



Msamaha huponya zaidi

NI wiki nyingine tena tunakutana nawe msomaji wangu kupitia safu hii kwa lengo la kupeana elimu na maarifa kuhusu masuala ya uhusiano.

Wiki hii nitazungumza umuhimu wa msamaha.

Msamaha ni dawa ya moyo uliojeruhiwa. Unapomsamehe mtu unapooza kidonda ambacho chuki na kinyongo vimeacha.

Watu wengi hubeba uchungu kwa miaka bila kujua kuwa mzigo huo unawaumiza zaidi wao wenyewe kuliko aliyekosea.

Msamaha unamfungua mtu kutoka gereza la hasira, unapunguza msongo wa mawazo, unaboresha usingizi na hata unaimarisha afya ya moyo. Mtu aliyejaa kinyongo huishi kwa hasira na huzuni, lakini yule aliyesamehe huishi kwa amani.

Katika uhusiano msamaha ni mafuta. Hata ndugu wanagombana, marafiki wakikosana, mwalimu na mwanafunzi wakikoseana, tiba pekee ni msamaha.

Bila msamaha uhusiano unakufa tarati-bu lakini ukiwepo, hata majeraha makubwa yanaweza kupona na upendo unarudi tena.

Kiroho msamaha una nguvu. Dini zote zinatufundisha kusamehe ili nasi tusamehewe. Msamaha pia ni ishara ya ukomavu na ujasiri, siyo udhaifu na unahitaji moyo mkubwa kuachilia na kuchagua amani.

Katika jamii nyingi watu wengi hukoseana na kuwekeana vinyongo, hushindwa kuelewana, hushindwa kuzungumza na ahata kusaidiana na chochote hata mmoja wao anapotokewa na tendo la huzuni au furaha. Wanakosea!

Msamaha si tu kwa ajili ya yule aliyekosea. Ni tiba kwako kwanza. Unapotoa msamaha unajiponya, unajikomboa, na unaruhusu furaha irudi moyoni mwako.

Tujifunze kusamehe ili kuruhusu amani kutawala mioyoni mwetu.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.

Mitindo & Urembo ■

Gauni la Maua Sama lilivyoteka hisia

MWANAMUZIKI Maua Sama ameteka hisia za mashabiki na wapenda mitindo mtandaoni baada ya kuonyesha muonekano wake wa gauni akiwa mjamzito.

Maua Sama ambaye tayari amejifungua, alionyesha ubunifu wa hali ya juu uliunganishwa na urembo kupitia gauni lake maalum.

Gauni hilo ambalo ni la muundo wa samaki na lisilo na mikono, limeshika mwili na tumbo lake likiwa katika muonekano nadhifu.

Vazi hilo pia lina nakshi za vipande vya mng'ao sehemu ya juu na limetengenezwa kwa kitambaa cha uwazi cha rangi ya mwili, kilichotiwa nakshi za kioo na mawe ya mng'ao zilizopangwa kwa mchoro ya ming'ao ya kipekee kifuani.

Ili kuongeza urembo amevaa mikufu ya fedha ya chuma ambayo imewekwa kwa ulinganifu kifuani na tumboni.



Fanya ngozi ya uso kuwa laini

NGOZI ya usoni inavutia kutokana na matunzo haswa kwa kufuata ratiba bora kuanzia namna ya kuosha hadi vitu unavyovitumia.

Hapa nimekuwekea vitu vingine vya kubusti mwonekano wako kama ifuatavyo;

* Tumia mafuta ya vaseline ya mgando kijiko kimoja na kiini cha yai.

* Osha vizuri uso wako kisha kausha vizuri.

* Changanya mafuta na kiini cha yai koroga vyema na upake usoni kwa kujimasage, kaa na mchanganyiko usoni kwa dakika 30, kisha nawa kwa maji safi ya uvuguvugu usitumie sabuni.

Fanya hivi mara mbili kwa wiki na utaona matokeo.

■ **Burudani**

Nandy amsaini Linah The African Princes

Na Mwandishi WETU

MSANII wa Bongo Fleva na mmiliki wa lebo ya The African Princess, Nandy, amemtambulisha rasmi msanii Linah kuungana naye.

Linah ametambulishwa katika lebo hiyo usiku wa kuamkia Septemba 4, 2026 katika ukumbi wa Mlimani City. Uzinduzi uliyoambatanisha na wimbo wa kwanza wa msanii huyo ulipewa jina la 'Raha.'

Akizungumza kati-ka uzinduzi huo, Nandy amesema katika safari yake ya muziki amekuwa akimfuatilia Linah kama role model wake.

"Linah ana kipaji kikubwa, nilikuwa najiuliza kwanini hatoi nyimbo wakati ana kipaji kikubwa? Nilikuwa namwuuliza lakini kuna siku akaja kunifungukia kwamba ana changamoto na amekata tamaa," amesema Nandy.

Priscilla 'alivyomsapraizi' Jux siku yake ya kuzaliwa

Na Mwandishi WETU

PRISCILLA, mke wa msanii wa Bongo Fleva, Juma Jux, amemfanyia surprise mumewe kwenye tukio la sherehe ya kumbukumbu ya siku ya kuzaliwa kwake.

Katika video aliyopost kwenye ukurasa wake wa Instagram, ilionyesha msanii huyo hakuwa anajua kinachoendelea hadi alipofika eneo la tukio.

Septemba 1, 2026 ilikwua ni kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Juma Jux hivyo tukio hilo ni moja kati ya tukio muhimu kwake akipewa zawadi na mke wake.



Utamu warejea Mwembeyanga

Na John MARWA

BAADA ya mapunziko ya wiki kadhaa, hatimaye utamu wa Ligi Kuu Mchezo wa Wavu Tanzania (TVNL 2026) umerejea Septemba, 06, 2026 katika Uwanja wa TVF uliopo Mwembeyanga, Tememeke jijini Dar es Salama kwa miamba ya klabu 24 kumenyana mzunguko wa pili.

Ligi hiyo, inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Wavu Tanzania (TVF) ilianza mzunguko wa kwanza mwanzoni mwa Agosti na kushuhudiwa upianzani mkubwa kwa klabu 14 za wanaume na 10 za wanawake.

Katika michezo aaba ya mzunguko wa kwanza kwa upande wa wanaume, Bandari VC walipata ushindi na kuongoza msimamo kwa pointi 20 pasipo kupoteza mchezo wowote. Nafasi ya pili ilishikiliwa na High Voltage kwa pointi 18, wakishinda sita na kupoteza mmoja.

Hali itakuwaje kwenye mzunguko wa pili kuelekea mzunguko wa tatu hadi fainali? Kinachozungumzwa hapa ni ufundi na vita ya kushinda michezo na seti zilizoko mbele yao.

Timu za Jeshi Stars, Nyika pamoja na JKT bado wanaweza kupindua msimamo kama Bandari VC na High Voltage hawatakuwa na mzunguko mzuri.

Kwa upande wa klabu za wananawake, Klabu ya Jeshi Stars ilihitimisha mzunguko wa kwanza ikiwa kinara kwa michezo mitano ambayo walishinda yote na kuvuna pointi 14, nafasi ya pili walikaa Tanzania Prisons pointi 13, michezo mitano wakishinda minne na kupoteza mmoja.

Wakati nafasi ya tatu kwa ukaribu, wapo Bandari VC na pointi zao 12 licha ya kushinda michezo minne kati ya mitano.

Swali sasa ni je, nani kumaliza vyema mzunguko wa pili na watatu hadi fainali?

Majibu yote yatapatikana pale TVF Arena, Mwembeyanga.

Ili kushuhudia magwiji wa mchezo huo, kila mpenzi anaombwa kwenda kutazama 'smash' za maana kutoka kwa wakali na 'master wa setters'.

Ukiachilia kurejea kwa burudani hiyo pend-



wa kwa wapenda mpira wa wavu nchini, kurejea kwa mzunguko wa pili kulisindikizwa na burudani mbalimbali kutoka kwa wasanii wa muziki nchini Tanzania wakiwamo Simba Mwala na K-Zungu, ambaye ni mkali wa free-style.

Mzunguko wa pili wa TVNL ulianza Septemba 6 na unatarajiwa kufika tamati Septemba 19 na kushuhudiwa mubashara kupitia Azam Sports 3 HD.



Mnyama anguruma, Wananchi si haba



Anicet Oura

Na John MARWA

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika (CAF CL) hatua za awali, Klabu ya Simba imeanza kampeni yao msimu wa 2026/27 kwa ushindi wa bao (0-1) dhidi ya Mighty Wanderers ugenini nchini Malawi.

Ushindi huo unaweka hai matumaini ya kusonga hatua za mtoano kuwania kutinga hatua ya makundi.

Mchezo huo ulipigwa Augosti 6, 2026 kati ka Dimba la Bingu, Uwanja wa Taifa la Malawi, na kushuhudia Simba, licha ya kupata matokeo

mazuri, walipata mchezo mgumu katika muda wa dakika zote 90.

Bao la Simba liliwekwa kambani na Anicet Oura baada ya kutumia vyema makosa ya walinzi wa Mighty Wanderers kushindwa kudhibiti mpira ulipigwa na mlinda lango Jibrila Kasali.

Kwa ushindi huo Simba inarejea nchini Tanzania ikiwa na kazi moja tu ya kumalizia dakika 90 za mkondo wa pili kupata ushindi wa jumla na kusonga mbele.

Wakati huohuo, Timu ya Yanga ilipata sare ya bao (1-1) dhidi ya Gaborone United, mchezo uliopigwa nchini Botswana Augosti 05, 2026.

Iliwahitaji Yanga SC kusubiri bao la Selemani Mwalimu dakika za nyongeza kipindi cha pili kuweza kusawazisha na kupata sare hiyo ugenini baada ya kutanguliwa na wenyeji wao kipindi cha kwanza kwa mpira wa ikabu.

Sare hiyo imeweka hai matumaini kwa Wananchi kya kusonga mbele hatua ya mtoano ambapo katika dakika 90 zitakazopigwa jijini Dar es Salaam wikiendi hii, Yanga watahitaji kupata ushindi ama suluhu ili kusonga mbele.

NI wazi si matokeo yaliyotarajiwa na mashabiki wengi wa miamba hiyo ya Soka la Tanzania kutokana na aina ya wapinzani wao, lakini mchezo wa kandanda unachezwa hadharani na kila mmoja kushuhudia namna ambavyo kete huchangwa na pande zote mbili.